SportPesa
TZS. 823,998,440
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#


UKURASA 3

## Joto la uchaguzi ACT-Wazalendo lapamba moto

ACT WAZALENDO

MAISHA Jumapili
Nipashe JANUARI 9, 2022 Baba, Mama na Mwana


SALAD YA NYAMA YA KUOKA


NYUMBA: Zingatia haya unapopanga nyumba


KATUNI


SUGUA GAGA
Tunza miguu kwa chumvi, asali

Jumapili Januari 9, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580820
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# MTIKISIKO

**Rais** Samia apangua Baraza la Mawaziri, vigogo watupwa nje, sura mpya zaibuka, wamo pia makatibu wakuu...
*Endelea ukurasa 2*

## WAPYA


Ridhiwani Kikwete


Nape Nnauye


Pindi Chana


Jumanne Sagini


Atupele Mwakibete


Dk. Stephen Kiluswa


Anthony Mavunde



Rais Samia Suluhu Hassan

## 'OUT'


Prof. Kitila Mkumbo


Prof. Palamagamba Kabudi


William Lukuvi


Geoffrey Mwambe


Mwita Waitara


Prof. Shukuru Manya

## WALIOPANDA


Angelina Mabula


Hamad Masauni


Hussein Bashe

## Mchakato kumpata Spika mpya Bunge uko namna hii

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA, YANGA ZILIVYOKAMATWA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Mtikisiko mabadiliko baraza la mawaziri

**Na Gwamaka Alipipi**

NI MTIKISIKO. Inaweza kuelezwa hivyo baada ya Rais Samia Suluhu Hassan jana kufanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara na Manaibu wao.

Mabadiliko hayo yameshuhudia baadhi ya vigogo waliokuwa vinara katika serikali ya awamu ya tano, chini ya Hayati John Magufuli wakitupwa nje na sura mpya kuibuka na wengine waliokuwa wamebwagwa wakirejea.

Uteuzi huo umefanywa zikiwa zimepita siku nne tangu Rais Samia alipotangaza kuwa atafanya mabadiliko muda wowote ili kuunda timu ya watu watakaoshirikiana naye katika kuwaletea maendeleo Watanzania.

Pia alisema atafanya mabadiliko hayo sababu kubwa ikiwa kuwaengua wale ambao wamejiingiza kwenye makundi ya Urais 2025 na kuwapa nafasi kuendelea na mbio zao badala ya kuharibu utendaji kazi wa kuwatumikia wananchi.

Hatimaye jana alitekeleza hilo kwa kuwaondoa mawaziri kadhaa waandamizi na kuwaingiza wengine wapya pamoja na kuwapandisha wengine kutoka unaibu waziri na kuwa mawaziri kamili.

Akitangaza mabadiliko hayo jana, Ikulu jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, alisema Rais Samia amefanya mabadiliko ya muundo katika wizara tatu.

Katika mabadiliko ya muundo huo, Rais Samia ameanzisha Wizara ya Uwekezaji Biashara na Viwanda. Awali kulikuwa na Wizara ya Viwanda na Biashara huku Uwekezaji ikiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Pia ameunda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Wizara ya Afya kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto," alisema Balozi Kattanga.

**MAWAZIRI WAPYA**

Katika mabadiliko hayo, Rais amemteua Nape Nnauye kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape alikuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika baraza la kwanza la Magufuli lakini akaachwa muda mfupi

Hamad Yussuf Masauni ameteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Dk. Pindi Chana kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). Kabla, Masauni alikuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

Dk. Angelina Mabula amekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi huku Hussein Bashe akiwa Waziri wa Kilimo. Dk. Mabula na Bashe walikuwa naibu mawaziri katika wizara hizo kabla ya uteuzi wa jana.

**MANAIBU WAPYA**

Katika mabadiliko yaliyotangazwa, Mbunge wa Dodoma Mjini, Peter Mavunde, anakuwa Naibu Waziri wa Kilimo na Jumanne Sagini, anakuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mavunde aliwahi kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Bunge, Sera, Uratibu, Kazi na Vijana wakati wa ngwe ya kwanza ya serikali ya Magufuli.

Sambamba na hao, Rais amemteua Ridhiwani Kikwete kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi huku Dk. Lemomo Kiruswa akiteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Madini. Atupele Mwakibete anakuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

**WALIOACHWA**

Katika mabadiliko hayo, Rais Samia amewaacha mawaziri vigogo kadhaa ambao baadhi yao katika awamu iliyopita, walikuwa katika chati za juu. Mmojawapo ni aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, pia aliwahi kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu) katika serikali ya awamu ya nne chini ya Rais mstaafu Jakaya Kikwete.

Waziri mwingine mwandamizi aliyetemwa kutokana na mabadiliko hayo ni Prof. Palamagamba Kabudi, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kabudi pia aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika serikali ya Magufuli.

Wengine walioachwa na wizara zao kwenye mabano ni Prof. Kitila Mkumbo (Viwanda na Biashara), Geoffrey Mwambe (Ofisi ya Waziri Mkuu- Uwekezaji), Prof. Shukuru Manya (Naibu Waziri wa Madini) na Mwita Waitara (Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi).



Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga.

**WALIOBADILISHWA**

Mbali na kuteuliwa wapya, kupandishwa na wengine kuachwa, mabadiliko hayo pia yamewagusa mawaziri na naibu mawaziri waliohamishwa.

Waliohamishwa ni Jenista Mhagama kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwenda Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ummy Mwalimu kuwa Waziri wa Afya kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na George Simbachawene kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kutoka Mambo ya Ndani ya Nchi.

Wengine ni Prof. Joyce Ndalichako kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi na Ajira, Innocent Bashungwa kutoka Michezo, Sanaa na Utamaduni kwenda Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Prof. Adolf Mkenda kutoka Kilimo kwenda Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Pia Dorothy Gwajima anakuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu. Awali, alikuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia. Wazee na Watoto ambayo zimeundwa wizara mbili.

Mohamed Mchengerwa anakuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Dk. Ashatu Kijaji anakuwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara kutoka Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**HAWAJAGUSWA**

Katika mabadiliko hayo, Balozi Kattanga alitangaza mawaziri ambao wamebaki katika wizara zao ambao ni George Mkuchika (Ofisi ya Rais Ikulu - Kazi Maalumu), Selemani Jafo (Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira) Dk. Mwigulu Nchemba ( Fedha na Mipango) na Dk. Stergomena Tax (Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa).

Wengine ni Balozi Liberata Mulamula (Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki), January Makamba (Nishati), Dk. Doto Biteko (Madini), Prof. Makame Mbarawa (Ujenzi na Uchukuzi), Jumaa Aweso (Maji) na Dk. Damas Ndumbaro (Maliasili na Utalii).

## Makatibu Wakuu, Manaibu waguswa

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana aliteua Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu katika wizara mbalimbali.

Mabadiliko hayo yaliyotangazwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, Ikulu jijini Dar es Salaam, yalielezwa kuwa ni ya kawaida katika kuimarisha utendaji wa kazi.

Balozi Kattanga, alisema Rais Samia amewapandisha waliokuwa Naibu Makatibu Wakuu na kuwa Makatibu Wakuu. Waliopandishwa ni Dk. Fancis Michael Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, awali alikuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Wengine ni Adolf Ndunguru anayekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Madini na amemteua Prof. Jamari Katundu kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Ajira, Vijana na wenye Ulemavu) ambaye kabla ya hapo alikuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali, Ndunguru alikuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango.

Pia Dk. Jim Yonazi ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari akiwa amepanda kutoka nafasi ya Naibu Katibu Mkuu katika wizara hiyo hiyo. Aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Kuwait, Mhandisi Aisha Amour anakuwa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi).

Naye Prof. Aliaman Sedoyeka ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia akitokea Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) alikokuwa Mkuu wa Chuo na Mhandisi Felchesmi Mramba, aliyekuwa Kamishna wa Nishati anakuwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati.

**NAIBU MAKATIBU WAKUU**

Exzavel Daudi aliyekuwa Katibu wa Sekretarieti ya ajira anakuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora huku Jenipher Christine akiteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango (Huduma na Hazina).

Wengine Lawrence Mafuru (Wizara ya Fedha na Mipango – Sera), Prof. Seif Shekilage (Wizara ya Afya), Abdallah Mitawi (Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano), Msafiri Mbibo (Madini), Juma Mkomi (Maliasili na Utalii), Dk. Filbert Mkama aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Russia (TAMISEMI), Said Yakoub (Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo), Ally Bungu (Uwekezaji, Viwanda na Biashara – Uwekezaji).

## NEMC yapiga marufuku vifungashio duni plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limepiga marufuku utengenezaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko na vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango kwa mujibu wa sheria, kwani kufanya hivyo ni kosa la Kisheria.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria, Redempta Samwel, alitoa tamko hilo jana Dar es Salaam kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Baraza baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika soko la Kisutu na Machinga, jijini Dar es Salaam.

Katika ziara yake, alibaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanajihusisha na uuzaji na usambazaji wa mifuko na vifungashio vya plastiki visivyokidhi vigezo.

Samwel alisema baada ya kufanya ukaguzi, zaidi ya viroba 50 vyenye vifungashio vya aina mbalimbali visivyokidhi viwango, vimekamatwa na vitaharibiwa na hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wanaohusika.

Kutokana na changamoto hiyo, alisema ni marufuku kutengeneza, kusambaza, kuuza au kutumia mifuko na vifungashio hivyo, kwa kuwa kufanya hivyo ni kukiuka sheria.

"Tumefanya ukaguzi na kukamata zaidi ya viroba 50 vyenye vifungashio vya aina mbalimbali vinavyotengenezwa hapa nchini visivyokidhi viwango. Viroba hivi vitaharibiwa na hatua kali za kisheria zitachuliwa dhidi ya wanaohusika na ukaguzi huu ni endelevu.

"Kwa Sheria ya Mazingira na Kanuni ya Kudhibiti Mifuko ya Plastiki ya Mwaka 2019, ni marufuku kutengeneza, kusambaza, kuuza au kutumia vifungashio visivyokidhi viwango, kufanya hivyo ni kukiuka kanuni ya katazo la mifuko ya plastiki. Kwa yeyote atakayebainika, tutamkamata na atachuliwa hatua za kisheria," alisema.

Sambamba na hilo, aliwataka Watanzania kuzingatia sheria, taratibu na kanuni ili kuepuka migogoro na serikali na kuepuka gharama zisizokua za lazima.

Naye Hamad Kissiwa, Meneja Kanda ya Mashariki Kusini, aliwataka wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kutokuzalisha, kutokupokea, kusambaza na kutumia mifuko na vifungashio visivyokuwa na viwango.

Alisema watengenezaji wa vifungashio visivyo na viwango hawalipi kodi na vifungashio hivyo vinauzwa kwa bei ya chini. Alisema kufanya hivyo ni kuikosesha serikali mapato na kudhoofisha biashara ya wananchi wanaotengeneza mifuko na vifungashio kwa kuzingatia viwango.

# Mchakato kumpata Spika mpya uko hivi

**Na Mary Geofrey**

SIKU tatu baada ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, kutangaza kujiuzulu nafasi hiyo, Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, ameeleza mchakato wa kumpata kiongozi mpya wa nafasi hiyo, utakaokamilika Februari Mosi, mwaka huu.

Mwihambi alisema jana kuwa katika kikao cha kwanza cha mkutano wa kwanza wa Bunge, baada ya kiti cha spika kuwa wazi, uchaguzi unaruhusiwa kufanyika kwa mujibu wa Katiba.

Alieleza utaratibu huo jana katika mahojiano yake na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), kuhusu mchakato wa kumpata spika mpya.

Mtu anayetaka kugombea nafasi ya spika, alisema, kwanza anatakiwa kwenda kuomba ridhaa kwenye chama chake na chama kikishapokea maombi ya watu, kitafanya mchakato wa ndani na kuteua jina moja litakalowasilishwa bungeni kwa ajili ya kushindana na wengine.

"Akishapatikana, katibu wa chama hicho anaandika barua kwa Katibu wa Bunge itakayoeleza jina la mgombea wa nafasi ya uspika, ambaye chama kimemteua," alisema Mwihambi.

Pia alisema Spika aliyejiuzulu, Ndugai, alipitishwa na chama chake, ndipo kikaandika barua kwenye ofisi ya Katibu wa Bunge.

"Katika utaratibu ule ule wa kutekeleza matakwa ya Katiba, ilibidi arudi kwenye chama chake kwa ajili ya kukieleza chama chake kuwa ameachia nafasi hiyo. Kwa utaratibu ule ule, alitakiwa arudi tena kwenye chama.

"Kwa maana hiyo ni lazima tena katibu wa chama arudi tena kwa Katibu wa Bunge kutueleza kuwa, yule tuliyemleta akagombea, akashinda uspika, sasa amejiuzulu na sisi chama tumeridhia kwa hiyo Bunge liendelee na utaratibu wake ili kumpata spika mwingine," alisisitiza Mwihambi.

Alisema kwa kufuata matakwa yale yale ya Katiba Ibara ya 149, Ibara ndogo ya 1 (C).

Mwihambi alisema taarifa hiyo itasomwa bungeni kwa muda mwafaka hadi hapo Bunge litakapokutana kwa mujibu wa katiba.

Alisema shughuli za Bunge zinaanza kwenye kamati na kwa sasa wameshatoa taarifa kwa wabunge kuwa kamati ambazo zilikuwa zikutane hazitakutana tena mpaka mkutano wa sita wa Bunge ambao utaanza Februari Mosi, atakapopatikana Spika mpya wa Bunge.

Mwihambi alisema baada ya hapo watatoa ushauri wa kuendeleza utaratibu uliowekwa na Bunge kuwa kamati zikianza asubuhi Bunge lianze saa 8:00 mchana.

"Kwa namna hiyo shughuli zilizokuwa zimepangwa kufanyika ndani ya hizi wiki mbili, zitafanyika na kukamilika kwa ukamilifu kabisa ndani ya kipindi hicho hicho," alisema.

**MCHAKATO SPIKA MPYA**

Akizungumzia uchaguzi wa kumpata spika kwa mujibu wa Katiba, alisema unafanyika katika nyakati kuu mbili.

Mwihambi alisema mosi, unafanyika wakati wa kikao cha kwanza cha mkutano wa kwanza wa Bunge, baada ya uchaguzi mkuu kufanyika.

Alisema yapo maelekezo mengine yametolewa kwenye katiba kwamba uchaguzi utafanyika kwenye kikao cha kwanza cha mkutano wa kwanza wa Bunge unaofanyika baada ya kiti cha Spika kuwa wazi.

"Kwa hiyo spika amejiuzulu mkutano unaofuata ni wa sita na unaanza tarehe moja mwezi wa pili, kikao cha kwanza cha mkutano huo ni tarehe moja, mwezi wa pili kwa hiyo ili kutimiza yale masharti ya katiba uchaguzi utafanyika tarehe moja mwezi wa pili," alisisitiza.

Kuhusu mchakato wa kugombea nafasi hiyo, alisema mtu yoyote anaweza kuwania kiti hicho, isipokuwa kuna mamlaka kisheria ambayo inaweza kuidhinisha mtu mwenye sifa ya kuwania kiti hicho cha Spika.

Mwihambi alisema: "Na mamlaka hiyo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwa hiyo kwa chama kinachotaka kumsimamisha atakayewania uspika na siyo mbunge kinatakiwa kupeleka jina hilo NEC siku tano kabla ya uchaguzi".



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama cha ACT- Wazalendo, Othman Masoud Othman (kushoto), akipokea fomu ya kuomba kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho kutoka kwa Naibu Katibu wa Idara ya Kampeni na Uchaguzi ya chama hicho, Muhene Said Rashid, Vuga Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Joto uchaguzi ACT- Wazalendo lapamba moto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JOTO za uchaguzi wa viongozi wa ngazi ya juu katika Chama cha ACT-Wazalendo, limezidi kupamba moto baada ya vigogo ndani ya chama hicho kujitosa kuwania nafasi mbalimbali.

Jana, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, alichukua fomu ya kuwania nafasi ya umakamu mwenyekiti wa chama hicho. Nafasi zinazogombewa ni ile ya Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo baada ya kuwa wazi tangu alipofariki dunia Maalim Seif Sharif Hamad Februari 17, mwaka jana. Maalim Seif pia alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Nafasi zingine ni ya makamu mwenyekiti wa chama hicho baada ya aliyekuwa anaishikilia, Juma Duni Haji, kutangaza kujiuzulu na kugombea nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu ya kugombea katika ofisi za chama hicho zilizoko Vuga, Zanzibar, Othman alisema anagombea nafasi hiyo ili kukitumikia na kukiimarisha chama.

Othman ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu wa ACT-Wazalendo, alisema licha ya chama chake kumwamini kushika nafasi ya Maalim Seif ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, haitakuwa kikwazo kwake kushindwa kutumikia nafasi anayogombea kwa sasa.

Alikiri kuwa baadhi ya maeneo yanahitaji nguvu za ziada katika kukiimarisha chama hicho ili kufikia malengo yanayokusudiwa ya kuleta mabadiliko ya kiutawala nchini.

Kwa mujibu wa Othman kuwapo kwa vyama vya siasa nchini ni jambo muhimu la kuongeza fikra bora zinazochangia kupatikana uongozi imara na serikali makini na hatimaye kuwaletea maendeleo wananchi.

Othman alisisitiza kwamba siasa za vyama vingi si uadui bali ni njia muhimu ya kuelekea ujenzi wa serikali imara sambamba na ishara za uwapo wa demokrasia katika nchi.

"Serikali imara inatokana na fikra imara na pia vyama imara, na wala siyo jambo la kugombana na kuleta uadui," alisema Othman.

Pia, alihimiza amani, umoja na mshikamano baina ya viongozi, wapenzi, wanachama na wafuasi wa ACT-Wazalendo, wakati huu na baada ya uchaguzi wa ndani wa chama hicho, kama ilivyokuwa kwa waasisi wake, akisisitiza kwamba kuna maisha baada ya uchaguzi.

Mjumbe wa Kamati ya Uchaguzi ya ACT-Wazalendo, Muhene Said Rashid, alisema lengo la uchaguzi ni kuwapata viongozi watakaosimamia na kuendeleza mema yaliyotokana na waasisi wa chama hicho.

Uchaguzi wa nafasi za Mwenyekiti wa Taifa na Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo upande wa Zanzibar, umepangwa kufanyika Januari 29, mwaka huu, Dar es Salaam.

HABARI KITAIFA

# Mradi mkubwa kumaliza kero sugu maji Dar

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Jijini Dar es Salaam (DAWASA), imeanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa usambazaji wa maji katika maeneo tisa Dar es Salaam, ambao unatarajiwa kumaliza kero ya upatikanaji huduma hiyo.

Mradi huo unaoanzia Gongo la Mboto, utapita maeneo ya Mtoni Kijichi, Chamazi, Mbagala, Kigamboni, Mianzini, Mbande, Kisewe na Posta na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 10. Mradi huo unatarajiwa kukamilika baadaye mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana Dar es Salaam na mwakilishi wa DAWASA, Mhandisi Lillian Masanago, wakati akisimamia utekelezaji wa mradi huo. Alisema mradi huo unatekelezwa kwa ufadhili wa fedha za Benki ya Dunia (WB).

Mhandisi Masanago alisema kwa kushirikiana na mkandarasi, watausimamia mradi huo kwa weledi ili ukamilike kwa wakati huku akisema utawasaidia wananchi kupunguza kero ya maji ambayo imekuwa sugu kwa muda mrefu.

"Tumefurahi sana kuanza huu mradi kwa maana tuna uhakika tutaenda kumtua mama ndoo ya maji kichwani na kumsaidia Rais (Samia Suluhu Hassan) katika jukumu la kuboresha maisha ya wananchi wa Dar es Salaam kwa kuwapatia maji safi na salama," alisema Masanago.

Aliongeza kuwa eneo la kwanza la utekelezaji wa mradi huo, zaidi ya wananchi 100,000 watanufaika na kwamba hawatasubiri hadi mradi ukamilike ndipo waanze kupata maji badala yake kila kipande kitakachokamilika wataruhusu huduma ya maji iweze kutolewa.

Pia aliwataka wananchi katika maeneo yaliyotajwa ambayo mradi unatarajiwa kupita, wakae tayari kupokea huduma ya maji na kuondokana na kero iliyokuwa ikiwakabili kwa muda mrefu.

Mkandarasi anayetekeleza mradi huo, Mhandisi Fredrick Mtoga, alisema mradi umegawanyika katika maeneo makuu matatu la kwanza likianzia Pugu, Gongo la Mboto kwenda Dovya, Kisewe hadi Chamazi.

Eneo la pili, kwa mujibu wa Mtoga, ni Mianzini, kwenda Mwanamtoti na vitongoji vyake na la tatu litaanzia eneo la Upendo mpaka Feri Posta na kwamba kutokana na mkataba, wanatakiwa kuukamilisha ndani ya miezi 12 kuanzia sasa.

"Tunachoweza kuwa ahidi kama wakandarasi na Watanzania tunajisikia uchungu na ni wazalendo, hivyo tutautekeleza mradi katika kiwango kizuri ambacho nyie wenyewe mtakikubali," alisema Mtoga.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wakiangalia mandhari ya bahari ya Hindi, baada ya mazungumzo yao, Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Dk. Mwinyi apongeza mafanikio vikao utatuzi kero za Muungano

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepongeza mafanikio makubwa yaliyopatikana katika vikao vya Muungano ikiwa ni pamoja na kutatuliwa mambo kadhaa.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu Zanzibar ilisema Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar alipofanya mazungumzo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kumpongeza kwa kumtembelea.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Mwinyi alipongeza usimamizi mzuri wa vikao hivyo vya Muungano ambavyo vimeleta tija na kutatua mambo kadhaa. Kati ya hoja 18, tayari 11 zimeshapatiwa ufumbuzi na kwa zile zilizobaki, ufumbuzi wake utapatikana ndani ya muda mfupi ujao.

Rais Mwinyi kwa mujibu wa taarifa hiyo, alitoa salamu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa ushirikiano mzuri uliopo hatua ambayo imekuwa na maslahi mazuri kwa pande zote mbili ikiwa ni pamoja na mgawo wa fedha za mkopo wa Shirika la Fedha Duniani (IMF), hatua ambayo itasaidia kujenga huduma za jamii na kuwapangia mipango wajasiriamali.

Alisema kuwa Serikali ya Muungano imekuwa na msaada mkubwa katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeridhika na hatua ya ushirikiano inayoendelea hali ambayo itasaidia kuimarisha na kukuza uchumi kwa pande zote mbili za Muungano.

Rais Dk. Mwinyi alitoa shukrani kutokana na nchi kuwa na amani na utulivu na kusema kwamba hatua hiyo ndiyo inayosababisha kuimarika kwa uchumi na kwamba kwa upande wa Zanzibar, utulivu umepatikana na wananchi wanashirikiana vyema na hivi sasa kuna kila sababu ya kupiga hatua kimaendeleo.

Pia alieleza UVIKO -19 ulivyoathiri uchumi wa Zanzibar na kueleza jinsi dalili za kuongezeka kwa watalii na kueleza haja ya Zanzibar kujifunza katika ukusanyaji wa mapato hasa baada ya janga hilo la maradhi kutokana na uchumi wa Zanzibar kuwa tegemezi kwa utalii.

Naye Waziri Mkuu Majaliwa alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kupata fursa ya kuiongoza Zanzibar nafasi ambayo anastahili na ameanza vizuri kuongoza kwani nchi imetulia na mahusiano ya Wazanzibari yamezidi kuimarika.

Alipongeza Rais Dk. Mwinyi anavyoshirikiana na Rais Samia na kuahidi kwa upande wao wasaidizi watapokea maelekezo yao na kusimamia majukumu ya kuwatumikia Watazania.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kumpongeza Dk. Mwinyi kwa jitihada zake za kuimarisha uchumi na hasa katika kuitumia fursa ya uchumi wa bluu na kueleza kwamba Tanzania Bara nayo itapanua wigo kutokana na sera hiyo aliyoiweka Dk. Mwinyi katika uchumi.

Waziri Mkuu alimhakikishia Rais Mwinyi kwamba juhudi za makusudi zitaendelea kuchukuliwa katika kuhakikisha vikao vya Muungano vinaleta tija na kuweza kuondoa changamoto zilizopo kwa haraka.

Pia alimhakikishia Dk. Mwinyi kwamba mamlaka za ukusanyaji wa kodi zitahakikisha zinakusanya mapato bila ya kutumia nguvu kwa lengo la kuwajengea imani Watanzania kwa serikali yao pamoja na kuwaamini viongozi wao wote ili nchi izidi kupata mafanikio.

Mapema, Rais Dk. Mwinyi alifanya mazungumzo na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Watu wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, Ikulu Zanzibar na kueleza kwamba serikali ya Zanzibar itahakikisha inawasaidia watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kuwajengea vyuo vya amali Unguja na Pemba ili wapate elimu za stadi za maisha.

Dk. Mwinyi alisisitiza kwamba unapotaka kumuwezesha mtu ni vyema ukampa elimu kwanza ili iweze kumsaidia katika kuendesha shughuli zake na ndio maana Serikali imeamua kuchukua hatua hiyo ya kutaka kuwajengea vyuo wajasiriamali.

Rais Dk. Mwinyi alisisitiza kwamba serikali zote mbili ile ya Muungano na ya Zanzibar zitafanya kila iwezekanavyo katika kuwasaidia na kuwaunga mkono watu wenye ulemavu.

Alieleza hatua na juhudi zinazochukuliwa na Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Wizara ya Afya katika kuwawekea mazingira mazuri na kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Rais Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kumpongeza Naibu Waziri Ummy kwa ziara yake aliyoifanya Unguja na Pemba sambamba na kuendeleza ushirikiano zaidi kati ya serikali zote mbili hasa katika wakati huu wa shamrashamra za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Naye Naibu Waziri Ummy alitoa salamu za watu wenye ulemavu alizopewa ili azifikishe kwa Rais Samia na Rais Mwinyi.

Alitoa pongezi kwa hatua za uteuzi ambazo amezifanya Rais Dk. Mwinyi kwa watu wenye ulemavu ambapo pia wakuu wa mikoa nao wameunga mkono juhudi hizo kwa kuwateua masheha ambao ni watu wenye ulemavu huku akieleza namna serikali zote mbili zilivyoweka mikakati ya kuwasaidia watu wenye ulemavu.

# HABARI KITAIFA

## Watumishi wa afya wafundwa uzalendo

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI Mkuu wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Meja Jenerali Dk. Gabriel Mhidze, amewataka watumishi wa afya nchini kuwa wazalendo katika kufanya kazi ili kutimiza azma ya serikali ya kuboresha afya za wananchi, kupitia miradi mbalimbali ya afya inayoanzishwa nchini.

Jenerali Mhidze alitoa rai hiyo juzi akiwa katika Hospitali ya Jeshi ya Lugalo mkoani Dar es Salaam, wakati akifunga mafunzo maalumu ya kusafisha damu (dialysis), yaliyotolewa kwa watumishi na wataalamu kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwananyamala.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imedhamiria kupunguza gharama za matibabu, kuboresha miundombinu ya afya, sambamba na kusogeza huduma mbalimbali za afya karibu na wananchi, ikiwamo huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo nchini.


Kwa mujibu wa Dk. Mhidze, lengo ni kuwajengea uwezo na umahiri katika kutumia mashine mpya na za kisasa zilizonunuliwa na MSD na zinatarajiwa kusambazwa katika hospitali mbalimbali nchini.

Mhidze aliwatunuku vyeti wahitimu hao na kuwataka kuwa mabalozi wazuri huko waendako, kwa kueneza mazuri waliyojifunza ili hospitali zingine kuhamasika na kuanzisha huduma hizo za kibingwa katika maeneno yao.

Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, alielezea ongezeko kubwa la wagonjwa wenye matatizo ya figo nchini na kuwataka wataalamu kufanya kazi zao kwa nidhamu na weledi ili lengo lililokusudiwa na serikali kupitia mafunzo hayo liweze kutimizwa.

Naye Mwakilishi wa wahitimu hao, Dk. Pantaleo Joseph, aliishukuru serikali kwa kuandaa mafunzo hayo adhimu, na kupongeza uongozi wa Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo.

Aidha, aliomba mafunzo hayo yawe endelevu na yawafikie wenzao walioko katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya, kwa sababu yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma na kuokoa maisha ya wananchi.




Meneja Mauzo wa Tigo Biharamulo, Amani Sailoja (kushoto), akikabidhi zawadi ya pikipiki kwa mkazi wa Forodhani, Flora Wilson Rutabingwa, baada ya kuibuka mshindi katika promosheni inayoendelea ya "wagiftishe gift juu ya gift", mjini Bukoba, mkoani Kagera juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Polisi, LATRA watoa mwarobaini tatizo la usafiri Kaskazini - Dar

**Na Waandishi Wetu**

HATIMAYE Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro, wamelipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa mabasi yaendayo Dar es Salaam yakitokea Moshi, baada ya kuruhusu baadhi ya mabasi madogo aina ya Toyota Coaster kuokoa jahazi, kwa kusafirisha abiria waliokuwa wakisota kituo kikuu cha mabasi tangu juzi.

Aidha, vyombo hivyo kwa nyakati tofauti, vimeeleza masikitiko yake kutokana na abiria hao kuficha taarifa za ongezeko la nauli za mabasi yaendayo mikoani hasa Tanga, Morogoro na Dar es Salaam, licha ya askari wa kikosi cha usalama barabarani, kubaini udanganyifu kwa safari za baadhi ya kampuni zinazotoa huduma za usafirishaji.

Jana, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Kilimanjaro, Paulo Michael, alisema tayari wameanza operesheni maalumu ya kukagua na kutoza faini mabasi yatakayoendelea kupandisha kiwango cha nauli kutoka Moshi hadi Dar es Salaam.

"Kwa sasa wasafiri wanaanza kupungua tangu jana, baada ya kuongezeka mabasi yanayokwenda Dar es Salaam yakitokea Moshi na Arusha. Yako ambayo tumeyapa vibali kwa ajili ya kupunguza utitiri wa abiria waliokwama kuondoka.

"Isipokuwa suala la ulanguzi wa tiketi za mabasi hatutakubali na tumeanza kuchukua hatua kali. Ni wajibu wa abiria kutoa taarifa kuhusu wanachoona hakiko sahihi hasa tiketi na nauli," alisema.

Kwa mujibu wa Ofisa huyo, tayari mamlaka hiyo imeweka vituo viwili vya ukaguzi katika kituo kikuu cha mabasi Moshi na kituo kidogo cha mabasi Same.

Kwa sasa, mawakala wa mabasi yanayofanya safari zake kati ya Moshi na Dar es Salaam wanalangua nauli kati ya Sh.30, 000 na Sh.45, 000.

Kuhusu abiria waliokwama kusafiri, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kilimanjaro (RTO), Zauda Mohamed, alisema mabasi yote yaliyoruhusiwa kuongeza nguvu ya kusafirisha abiria hao yanafanyiwa ukaguzi kwanza ili kupata uhakika wa safari.

Katika mkoa wa Arusha, abiria wanaosafiri kutoka mikoa ya Manyara na Arusha, wao wameipongeza LATRA, kwa kutoa kibali kwa mabasi madogo aina ya Toyota Coaster na mabasi ya kati, kupeleka abiria Dar es Salaam.

Alipoulizwa kuhusiana na uamuzi huo, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Arusha, Amani Mwakalebela, alisema mamlaka hiyo imeshafungua milango kwa wenye mabasi yaliyokaguliwa kuomba kibali cha kusafirisha abiria kutoka Arusha kwenda Dar es Salaam.

"Bado kuna shida kubwa ya wasafirishaji kujitokeza. Wanaokuja ni wachache kuliko matarajio yetu na wasafiri kwa ujumla wao. Tunawaomba waje kuokoa jahazi,"alisisitiza Mwakalebela

Mmoja wa wasafiri hao, Amina Makiungu, alisema kwa sasa hali imeanza kubadilika na wamepata usafiri wa kurejesha makwao Jijini Dar es Salaam, kwa kuwa mwanzo waliona hakuna namna wangeweza kuepuka ulanguzi wa tiketi pamoja na kutoa Sh.5,000 kwa wakala wa mabasi ili akushikie nafasi ya kiti kwenye basi.

■**Imeandikwa na Mary Mosha (MOSHI) na Tumaini Mafie (ARUSHA)***

## Morogoro kicheko kukamilisha ujenzi madarasa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

VYUMBA 707 vya madarasa ya shule za sekondari na 142 vya shule shikizi za msingi mkoani Morogoro vimekamilika kwa asilimia 100 tangu Desemba 31, mwaka jana, kwa ajili ya wanafunzi 54,366 kuanza rasmi shule Januari 17.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Mariam Mtunguja, alisema hayo jana wakati akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu na afya chini ya mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Mtunguja alisema vyumba hivyo vya madarasa vyote vimekamilika sambamba na kutengenezwa kwa madawati 24,624 ambayo yalikuwa pungufu kwa shule zote.

Alisema mkoa wa Morogoro ulipokea Sh. 20,250,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu na afya chini ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19. Alisema katika sekta ya elimu, zilielekezwa Sh. 17,060,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 849 vya madarasa.

Pia alisema Sh. milioni 80 zilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja katika shule ya msingi yenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu wilayani Mvomero.

Mtunguja alisema uhitaji wa vyumba hivyo vya madarasa umetokana na matokeo ya ufaulu wa wanafunzi kimkoa mwaka 2021 ambao ni wanafunzi 54,366 sawa na asilimia 91 ya wanafunzi 59,749 waliofanya mitihani, hivyo kufanya kuwa na mahitaji ya madarasa 1,139 na madarasa yaliyokuwapo yalikuwa 432 na kuwa na upungufu wa madarasa 707.

Alisema fedha hizo pia zimewezesha ujenzi wa ofisi sita za walimu na kuwa na bakaa ya Sh. 130,538,863.13 kutoka katika halmashauri zote mkoani hapa.

Kuhusu fedha za Sekta ya Afya, alisema Sh. bilioni 3.19 zimepokewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 18 ya uboreshaji wa miundombinu ya afya ambayo ni ujenzi wa vituo vinne vya huduma za dharura, ujenzi wa chumba kimoja cha wagonjwa mahututi (ICU) kitakachojengwa Halmashauri ya Wilaya Kilosa.

Shughuli zingine ni ujenzi wa nyumba saba za tatu kwa moja kwa watumishi wa afya vitakavyogharimu Sh. bilioni 1.930 na upanuzi wa X-RAY tatu kwa thamani ya Sh. bilioni 1.26 miradi ambayo kwa sasa iko katika hatua ya kutia saini mikataba na makandarasi.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Halima Okash, alisema kupitia Sh. milioni 2.44, madarasa 122 yakiwamo 15 ya shule shikizi, yamekamilika kwa asilimia 100 na wako tayari kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza na kuepukana na adha ya kuchangishana kwa ajili ya madarasa ya wanafunzi.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Kipera, Mlali wilayani Mvomero, Anna Kazimoto, alisema wamekamilisha ujenzi kwa asilimia 100 wa madarasa tisa yaliyotakiwa kupitia Sh. milioni 180 walizopokea kutoka serikalini sambamba na kupata madawati kwa kila darasa kuwa na madawati 50.

Alisema ujenzi wa madarasa hayo utaboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi na kufundishia kwa walimu na kwenda kuondoa msongamano wa wanafunzi madarasani na kuwaondolea wengine adha ya kukaa chini na hivyo kutarajia kuwa na ufaulu mzuri.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko mapya Baraza la Mawaziri yalete tija

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, jana alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri zikiwa ni takriban siku nne tangu alipotangaza kuwa anakusudia kutekeleza hilo.

Samia alitangaza nia ya kufanya hivyo mapema wiki hii, huku akiweka mkazo kuwa anaisuka timu itakayomsaidia katika kuwaletea maendeleo Watanzania katika sekta mbalimbali kama alivyoapa wakati akichukua nafasi hiyo machi 19, mwaka jana, akichukua nafasi ya aliyekuwa mtangulizi wake, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia.

Licha ya kulisuka baraza hilo la mawaziri, Rais pia alitangaza uteuzi wa makatibu wakuu wa wizara mbalimbali wakiwamo waliokuwa naibu makatibu wakuu na makatibu tawala wa mikoa huku akiwahamisha baadhi kutoka wizara moja kwenda nyingine.

Katika mabadiliko ya baraza la mawaziri, Rais Samia aliwateua baadhi ya wabunge kuwa mawaziri na naibu mawaziri huku baadhi ya waliokuwa naibu mawaziri wakipandishwa kuwa mawaziri kamili. Pia aliwaacha mawaziri watano wakiwamo wawili waandamizi na naibu mawaziri wawili. Sambamba na kufanya hivyo, aliwahamisha baadhi ya mawaziri na naibu mawaziri kwenda wizara nyingine huku wengine wakibaki katika wizara walizokuwamo.

Kwa ujumla mabadiliko hayo yameonyesha dhamira ya dhati ya Rais Samia ya kutekeleza ahadi zilizotolewa wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aidha, kama alivyosema wakati akitangaza kusudio la kufanya hivyo kwamba anataka timu itakayo kwenda naye sambamba katika kuwatumikia wananchi na kuwaweka pembeni baadhi ya mawaziri na viongozi waliojiunga katika makundi kwa ajili ya mbio za urais katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025.

Wakati akitangaza kusudio hilo, alisema bayana kwamba anataka kuwa na mawaziri na watendaji ambao watatekeleza kwa dhati mipango ya serikali kwa ajili ya maendeleo kupitia sekta mbalimbali, kama vile elimu, afya, miundombinu na maji.

Ni wazi kwamba timu hiyo iliyosukwa, ambayo wateule wapya wataanza kazi rasmi baada ya kuapishwa kesho, ina mchanganyiko wa watu ambao wanaonekana dhahiri kuwa watatekeleza majukumu yao kisekta na kutimiza maono ya Rais kama ilivyokusudiwa.


Aidha, mawaziri hao na manaibu wao pamoja na makatibu wakuu walioteuliwa, wanaonekana kuwa na uwezo katika kutekeleza maono ya aliyewateua, hivyo wanatakiwa wafanye kazi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu. Tunasema hivyo kwa sababu kumekuwa na malalamiko katika baadhi ya maeneo kuwa miongoni mwa watu wanaoteuliwa kushika nafasi za uongozi, wanatumia madaraka yao kujinufaisha au kama fimbo ya kuwapigia watu walio chini yao.

Hata hivyo, ni imani yetu kwamba hadi rais kufikia hatua ya kuwateua katika nyadhifa hizo na wengine kupandishwa na kuhamishiwa kwenye maeneo mengine, wameaminiwa kuwa wana uwezo wa kukidhi matarajio ya uongozi wa juu wa nchi chini ya Rais Samia.

Kwa mantiki hiyo, wanachotakiwa ni kuonyesha kuwa wana uwezo katika kutekeleza majukumu yao pamoja na kuwa wabunifu katika mambo yanayohusu sekta zilizo chini ya wizara zao.

Sambamba na kuonyesha kuwa wana uwezo katika kutenda, pia watambue kwamba hawapo katika nafasi hizo milele bali wanaweza kuondolewa wakati wowote kama walivyofanywa baadhi ya walioenguliwa. Jambo pekee litakalowafanya kuendelea kuwamo katika timu ya uongozi ni utendaji wao na kufuata misingi ya viapo vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Fursa katika mitandao ya kijamii zisiachwe zipotee



Na Sabato Kasika

**VIJANA** wamekuwa wakitajwa kutumia mitandao ya kijamii kwa wingi lakini pia wanadaiwa kuwa vinara wa kutumia vibaya mitandao hiyo, hali ambayo inaweza kusababisha kuingia kwenye matatizo.

Mitandao hiyo imekuwa sehemu si tu ya kimawasiliano bali pia kimaendeleo katika jamii nyingi, hasa miongoni mwa vijana katika mataifa mbalimbali ikiwamo Tanzania.

Kuwapo kwa mitandao hiyo kumekuwa pia kukisaidia watu kupata taarifa mbalimbali kwa urahisi na tena kwa wakati, na ina fursa nyingi zikiwamo za watu kupata ajira kutangaza biashara zao na mambo mengine muhimu.

Vilevile mitandao imekuwa ikitumiwa kuhamasisha shughuli mbalimbali zikiwamo za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pamoja na mitandao hiyo kuwa na fursa hizo, inaelezwa kuwa wako baadhi ya watu wanaitumia vibaya.

Linapojitokeza suala kwamba baadhi ya vijana wanaitumia vibaya, basi kuna haja ya wao kutafakari na kuchukua hatua zitakazowasaidia kuepuka mtindo huo ili wasije kuingia katika matatizo. Ninaamini kwamba kupitia mitandao ya kijamii, vijana wanaweza kujifunza mambo mengi mazuri yakiwamo yanayohusiana na uongozi, wanaweza kufahamu kiongozi ni nani na kiongozi ana sifa gani.

Pia wanaweza kufahamu kiongozi anafanya nini na kwa wakati gani ili nao kujiandaa kwa ajili ya kuwa viongozi wa kesho badala ya kujikita kwenye mijadala ambayo inaweza kusababisha wakajikuta kwenye matatizo.

Ingependeza iwapo vijana watashinda mitandaoni wakitafuta fursa mbalimbali kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla kuliko kuanzisha mijadala ambayo haina afya kwa jamii na taifa lao kwa ujumla.

Jambo la msingi ni kutumia uhuru wa kutoa maoni, kushauri kwa usahihi ili jamii iweze kunufaika navyo, na kujiweka kando na yote ambayo yanaweza kusababisha vijana wasione hawana umuhimu kwa nchi yao.

Uandikaji wa taarifa za uchochezi ni miongoni mwa matumizi mabaya ya mitandao hiyo. Hata Rais Samia Suluhu Hassan amewahi kukemea na kuwataka Watanzania kuacha mara moja mtindo huo.

Rais aliwataka waitumie inavyotakiwa ili kunufaika nayo na kwamba amekuwa akifuatilia mitandao na kuona yanayoendelea, na kusema hayafurahishi, kwa kuwa ni mambo yanayochonganisha wananchi.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, naye amewahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema serikali inakusudia kuweka mfumo wa kudhibiti mijadala isiyofaa.

Uamuzi huo unakwenda sambamba na kuwachukulia hatua wale wote wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii, hasa Facebook na Instagram ambayo imekuwa ikikusanya watu wengi hasa vijana.

Kwa mujibu wa waziri huyo, watu hao hawawezi kuachwa waendelee bila utaratibu kwa madai kwamba, wanaweza kuleta uvunjifu wa amani kutokana na kukashifu viongozi wa serikali.

Ni kweli kwamba mitandao hiyo inadaiwa kukusanya watu wengi na inawezekana wengi wao ni vijana, hivyo inawezekana kuna haja ya kuweka utaratibu ili kufuatwa kuliko kuachwa wakifanya wanavyotaka.

Iwapo hayo yana ukweli, basi ni dhahiri kwamba, kuna haja ya watu kutumia vizuri mitandao hiyo, kwa ajili ya maendeleo ya nchi na pia kuimarisha amani na mshikamano wa Watanzania.

Pamoja na hayo, ni vyema vijana kuzingatia lengo namba 16 la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa (SDG), ambalo linachagiza jamii zenye amani na jumuishi, hivyo si vibaya wanaotumia mitandao hiyo kuchagiza umuhimu wa kuifanya Tanzania kuendelea kuwa nchi ya amani.

# SAFU/MAKALA

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tujenge utamaduni wa uwajibikaji kumpunguzia Rais mzigo wa karma



Na Pascal Mayalla

KWA kadri ya siku zinavyokwenda, wale watu wa Nyerere wanazidi kupungua katika kizazi cha sasa. Waliokuwa wanaujua utawala wa Mwalimu Julius Nyerere ni wachache, wengi ni kizazi kipya cha utawala wa Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete na John Magufuli.

Inawezekana kabisa wengi wasielewe kuwa enzi za Nyerere, viongozi wetu walipofanya makosa ya wazi, si tuu waliomba msamaha, bali msamaha huo uliandamana na barua ya kuwajibika.

Kwa hiyo nauliza kwa viongozi wetu hawa wa sasa pale wanapofanya makosa ya wazi kabisa, au makosa ya kujikwaa kisiasa, je, tuwaache waombe tu msamaha na maisha kuendelea kama kawaida? Au sasa tujenge utamaduni wa viongozi wetu wanapofanya makosa, hata kupishana tu kauli na mkuu wa nchi, kuwajibika kwa makosa yao na wasiishie kuomba tu msamaha tena misamaha mingine ni batili. Mtu unafanya kosa la wazi badala ya kuomba tu msamaha na kusema ulighafilika, wewe unaanza kwanza kwa kutoa visingizio vya eti nilinukuliwa vibaya! Au nimebambikiwa maneno hayo, ndipo unaomba samahani.

Ili kujenga nidhamu ya kweli ya uwajibikaji, pale kiongozi anapokosa, asiishie kuomba msamaha tu, bali msamaha huo uandamane na barua ya kuwajibika kama enzi za Nyerere.

Mfano mzuri wa ombi la msamaha likiandamana na uwajibikaji ni kujiuzulu kwa Mzee Mwinyi, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi enzi hizo kutokana na vifo vya mahabusu wakiwa mikononi mwa polisi vilivyotokea mwaka 1976 mkoani Mwanza na Shinyanga. Mwaka 1977, Mwinyi aliandika barua kwa Rais Mwalimu Nyerere ya kuomba msamaha na kuwajibika.

Tena kwenye kadhia hiyo, haikuishia kwa Mwinyi pekee kujiuzulu, bali Rashidi Kawawa aliondolewa kwenye Umakamu wa Pili wa Rais kwani pia Waziri wa Usalama wa Taifa, Peter Siyovelwa alijiuzulu. Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa, Emilio Mzena alistaafishwa, Mkuu wa Jeshi la Polisi Inspekta Jenerali (IGP), Samuel Pundugu alistaafishwa, Kamisha Mkuu wa Magereza alistaafishwa.

Licha ya vigogo hao, moto huo ulihamia Mwanza. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Peter Kisumo, alimwaga unga. Kamanda wa Polisi wa Mkoa (RPC), Ofisa Usalama wa Mkoa (RSO), Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) na Mkuu wa Wilaya ya Mwanza si tuu walimwaga unga bali kwa kustaafishwa kwa manufaa ya umma.

Nikiwa mtoto wa mmoja wa maofisa hao, Mzee Andrew Mayalla (baba yangu sasa marehemu) alisema si tu unastaafishwa na kuamua kuishi popote, bali unastaafishwa na kufuatwa usiku usiku kusafirishwa kurudishwa kijijini kwenu kwa Landrover 109 za enzi hizo na baba kukabidhiwa kwa serikali ya kijiji, huruhusiwi kutoka nje ya kijiji bila ruhusa!.

Mtu ulikuwa ni mtoto wa bosi, ukipelekwa shule kwa gari la kazini kwa bosi, mara ghafla mnarudishwa kijijini kuwa wanakijiji wa kijiji cha ujamaa. Haikuishia hapo, maofisa hao walifikishwa mahakamani kwenye ile "Kesi ya Mauaji Mwanza" tena maofisa wa baadhi ya idara za serikali wa enzi hizo, mpaka niko darasa la nne, ndio nakuja kujua Mzee Mayalla alikuwa nani tena kwa kusoma kwenye gazeti la Mzalendo. Lakini maofisa wa siku hizi, wanatambia nafasi zao hadi kugombea mabibi baa! Ukimshinda unaonyeshwa yeye nani!

Maofisa wote walihukumiwa vifungo virefu isipokuwa mshtakiwa mmoja tu, Mzee Mayalla, yeye ndiye pekee alikutwa hana hatia nadhani ni kwa sababu alikuwa anatetewa na wakili mahiri, Murtaza Lakha, ndiye aliemwokoa.

Huu uwajibikaji wa enzi za Mwalimu, umepotelea wapi?. Mahabusu wangapi siku hizi wanakufa mikononi mwa polisi na hakuna uchunguzi wowote wala mtu yeyote anayewajibika?

Hivi majuzi Mkuu wa Mhimili wa Bunge ametofautiana na Rais katika jambo la kweli na la msingi kabisa kuhusu mikopo na deni la taifa. Kiongozi huyu badala ya kusimama kwenye hoja yake na kujiuzulu kwa heshima kwa kutofautiana na bosi wake, akaamua, si kuandika barua ya kuomba msamaha, bali kuita waandishi na Bunge kulipia matangazo ya moja kwa moja na kuomba msamaha mubashara kwenye runinga. Kwa nini asingetangaza kujiuzulu kwa heshima?.

Mwombaji msamaha badala ya kukiri tu kosa, akatafuta visingizio vya uongo, hivyo kuufanya msamaha wake kuwa batilifu, bila ubatilifu kuondolewa, ukawa msamaha batili na ukakataliwa, hivyo ndio kulazimika kujiuzulu kwa aibu.

Tena ule msamaha batili haukuishia kwenye msamaha tu, hata taarifa kwa vyombo vya habari, kuhusu kujiuzulu, kunaonyesha barua ya kujiuzulu imeandikwa kwa Katibu Mkuu wa CCM nakala kwa Bunge badala ya Katibu wa Bunge nakala kwa CCM!. Hii ni barua batili ya kujiuzulu. Bunge letu lilivyo la ajabu, limekubali nakala ya barua hiyo batili na kutangaza limeipokea!. Kama katiba imeelekeza jinsi ya kujiuzulu Spika na utaratibu, kwa nini ifanyike batili na kuruhusiwa na chombo cha juu kama Bunge?

Kwenye hutuba ya Rais Samia, kuna kiongozi mwingine ametajwa kujihusisha na harakati za urais wa 2025. Tufike mahali viongozi wetu wa kisiasa wawe na viwango vya uadilifu vya mke wa Kaisari. Hata ukituhumiwa tu hata kama si kweli, ile kutuhumiwa tu, unakaa pembeni, halafu kama si kweli, si utaitwa tena?

Samia alipoingia, tulimshauri kiongozi mmoja mkubwa tu ajiuzulu ili kumpa Samia fursa ya kuisuka timu yake, halafu kama bado anahitajika si atateuliwa tena?. Sasa jina la kiongozi huyo limetajwa tena! Rais Samia kasema hivi karibuni atafanya panga pangua nyingine, hivi huyu kiongozi anasubiri nini mpaka sasa kuwajibika na kupisha ili kumpa mama fursa ya kuunda timu yake?. Kama bado anahitajika, si ataitwa tena?

Ni lini uwajibikaji kwa viongozi wa umma utarejeshwa kwa kiwango cha uwajibikaji wa enzi za Mwalimu? Kiongozi wa umma ni mpaka afanye kosa kubwa gani ndipo awajibike? Kitendo cha Rais kutumbua, kunasababisha kumbebesha Rais wetu kitu kinachoitwa "karma", hivyo viongozi mnapofanya makosa ya wazi wajibikeni kumpunguzia Rais wetu mzigo wa karma.

**Nitaendesha na somo la "karma" wiki ijayo.**

**Paskali. Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kwa kweli hii ni kwa mara ya kwanza



Na Joseph Kulangwa

KILA mmoja kauanza mwaka huu wa 2022 kivyakevyake. Kwa mwenzetu Job Ndugai kauanza na hisia tofauti kutoka kwa watu tofauti. Wako wanaoshangilia kilichomtokea ambao ni wengi, lakini wapo wanaosikitika na kumsikitikia ambao ni wachache.

Sina takwimu, lakini upepo unaonesha dhahiri kuwa watu wanashangilia kuondoka kwake kama Mkuu wa Mhimili wa tatu wa Dola-Bunge. Sijui inatokana na nini lakini bila shaka huwezi kupanda mtende ukavuna embe.

Siku zote wanasema mpandaji huvuna alichokipanda. Hivyo bila, shaka Ndugai alichokivuna ndicho alichokipanda. Vivyo hivyo semi nyingi za Kiswahili zimekuwa zikihanikiza haya na yale. Utawasikia wengine wakisema kuchamba kwingi...

Semi ziko nyingi zinazo akisi kilichomkuta jamaa yetu huyu ambaye alishajinasibisha kuwa ni yeye na yeye ni Bunge na hakuna mtu wa kumtingisha hata iweje, ndiyo maana kuna siku akapiga mkwara, kuwa anaweza kumfanya lolote mbunge yeyote na asimfanye chochote. "Pambana na kitu ingine lakini si Ndugai," alimalizia.

Tukio lake la kujiuzulu, limeacha funzo kwa wengi, kwamba cheo ni dhamana tu. Leo upo kesho haupo na anakuja mwingine anakalia kiti hichohicho na mambo yanasonga mbele na kazi inaendelea. Pengine hii ndiyo inafanya watu wengi wanafurahia yaliyomkuta Ndugai.

Mimi siko kokote kati ya pande hizo mbili lakini ninahisi kuwa upande mmoja kati ya hizo. Kwa sababu inawezekana alisema ukweli katika jukwaa lile la Wagogo lakini kwa nini akaja kusema kalishwa maneno na baadaye jioni, akaomba radhi kuwa amekosa yeye na amekosa sana?

Wanaoamini kwamba alisema ukweli kuhusu madeni lakini wanashangilia kuondoka kwake, basi walikuwa na sababu zingine tu nje ya kauli hiyo na walikuwa wakimtafutia mahali anase wasimnasue na washangilie kwa vinubi na zumari kama inavyofanyika.

Ila pamoja na yoote hayo, Ndugai amesaidia kuiandikia Tanzania hitoria iliyotukuka kwamba kwa mara ya kwanza, Spika wa Bunge anajiuzulu katika historia ya Tanzania kama ilivyokuwa kwa mara ya kwanza, Tanzania inafiwa na Rais aliyeko madarakani.

Kama ilivyokuwa kwamba kwa mara ya kwanza Tanzania inapata Rais mwanamke katika historia yake na kwamba kwa mara ya kwanza, Tanzania inapata Waziri wa Ulinzi mwanamke. Na kwa mara ya kwanza, Tanzania inapandisha bei ya kuingiza umeme majumbani kutoka Sh 27,000 mpaka milioni na nusu na ushei!

Lakini pia kwa mara ya kwanza kabisa, Disii anafungwa miaka 30 jela kwa ujambazi na unyang'anyi. Sikumbuki, lakini nadhani ni kwa mara ya kwanza. Tanzania inajiandikia historia yake iliyotukuka ambayo bila shaka wajukuu na vitukuu na hata vilembwe na vilembwekezi vitakuja kuisoma.

Mimi nimpe pole na kongole Ndugai kwa yote aliyoyafanya na yaliyomkuta na kumpa moyo atumaini ya mbeleni, kwa sababu kajikwaa akaanguka, lakini bila shaka keshasimama na sasa alipiganie jimbo lake la Kongwa, kama ambavyo alikuwa kabla hajakalia kiti hicho kitamu.

Kwa sisi kajamba nani tulioko huku uraiani tuendelee kujifunza kwa wenzetu waliotutangulia, ambao si pangu pakavu tia mchuzi. Tunaowapa madaraka kwa ama kuwachagua kwa kura au kwa kuteuliwa na tuliowachagua, kwamba tabia njema ni silaha katika maisha.

Tusipewe dhamana tukadhani tumefika na kujisahau kuwa pengine madaraka tuliyonayo yatakoma siku ya kiyama, siku atakaporejea Masiah na kutuchukua ndipo atachukua na madaraka yetu. Sivyo, kila mtu na muda wake na kila dhamana na wakati wake.

Tunachokishuhudia hivi sasa ni matokeo ya kujisahau tu na pengine jeuri kidogo. Tuliwaona kina Ole wakifanya yao kuanzia Hai mpaka Arusha na matokeo yake, yakawa kama hivyo miaka 30 jela.

Tulishuhudia baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa, wakijiamulia mambo yao tu kwa hisia na matakwa yao, na kunyanyasa watu ama kwa kuwapiga au kuwapora vilivyo vyao, huku wakijinasibu hakuna wa kuwagusa. Iliwezekana wakati huo lakini si leo. Yajayo chini ya Chifu Hangaya yanafurahisha, yetu macho na masikio.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Maofisa waliohusika kuingiza chumvi feki wachukuliwe hatua



Na Thobias Mwanakatwe

NGORONGORO ni moja kati ya halmashauri za wilaya sita na jiji moja katika mkoa wa Arusha. Makao makuu ya wilaya yako Loliondo Wasso umbali wa takriban kilomita 400 kutoka Arusha mjini ambako ni makao makuu ya mkoa.

Wilaya hii ilianzishwa mwaka 1979 chini ya Sheria Namba 5 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 ikiwa na tarafa za Loliondo, Sale na Ngorongoro.

Tarafa ya Ngorongoro imo kwenye eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) iliyoanzishwa kwa Sheria Sura 413 ya mwaka 1959 (NCA, CAP 284 (R.E.2002) na linasimamiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA). Zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa wilaya ya Ngorongoro ni wafugaji na maisha yao wanayaendesha kwa kutegemea mifugo.

Wafugaji katika wilaya hii kwa miaka yote wamekuwa wakilisha au kuchunga mifugo yao ndani ya bonde la Hifadhi ya Ngorongoro kwa sababu eneo hilo yanapatikana maji na chumvi ya asili inayopendwa na mifugo.

Hata hivyo, mwaka 2016, serikali iliamua kupiga marufuku wafugaji kupeleka mifugo yao ndani ya bonde la Ngorongoro ili lisiharibiwe na mifugo hasa ikizingatiwa kuwa bonde hilo ni kivutio muhimu cha watalii ambao kila mwaka wamekuwa wakimiminika hapo.

Kwa kuthamini wafugaji na kujenga uhusiano mzuri, serikali iliagiza NCAA iwe inawapatia chumvi wafugaji kwa ajili ya kulishia mifugo yao. Utekelezaji huo ulianza tangu mwaka 2017.

Hata hivyo, mwishoni mwa mwaka jana, kuliibuka malalamiko ya wafugaji ambao walidai chumvi waliyoletewa na NCAA haina ubora na inahatarisha maisha ya mifugo yao. Chumvi hiyo ambayo ilizua utata, inadaiwa imesambazwa kwa wafugaji hao na NCAA waliodai ilikuwa imechanganywa na mawe na rangi na mwanyama wanapotumia, wanaharisha, hivyo kuhatarisha afya za ng'ombe hao.

Diwani wa Kata ya Ngorongoro, Simon Saitoti, alisema hali si nzuri kwa mifugo ya wafugaji wa kata hiyo baada ya kuitumia chumvi hiyo ambayo inadaiwa kununuliwa kutoka nchi jirani. Saitoti akasema katika kata yake ililetwa mifuko 900 na imeshasambazwa kwa zaidi ya wafugaji 5,000 na kubakia sita tu kupitia kwa wenyeviti wa vijiji na kwamba baada ya ng'ombe kuanza kuitumia, wakaanza kuona dalili tofauti.

Alisema baada ya kupelekewa malalamiko na wafugaji, naye alitoa taarifa kwa ofisa mifugo na viongozi wa NCAA. Baada ya hapo kiliitishwa kikao cha wenyeviti wa vijiji vya Kayapusi, Ololilobi na Mokilale. Kikao hicho kilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala.

Mangwala kwa upande wake baada ya kuona malalamiko yamezidi, aliagiza chumvi hiyo isiendelee kutolewa kwa wafugaji tena na wale ambao wamekwishapewa wasiipe mifugo. Pia aliagiza ipelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ili ufanyike uchunguzi wa kisayansi.

Kwanza, nianze kwa kupongeza uamuzi wa serikali ya wilaya ya Ngorongoro kwa kuamuru chumvi hiyo ipelekwe kupimwa kujua kama inafaa kwa matumizi ya mifugo au la.

Maofisa watatu kutoka NCAA akiwemo Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Ngorongoro, Dk Chobi Chubwa na Saitoti, nao waliungana katika jopo hilo kupeleka sampuli hiyo Dar es Salaam.

Kabla ya kuanza safari ya kuelekea Dar es Salaam jopo la maofisa hao lilifanya mahojiano na mmiliki wa kampuni ya Panga Building Materials and Company Limited, Mark Panga, ambaye kampuni yake ilipewa zabuni ya kununua chumvi na NCAA.

Katika mahojiano hayo, Panga aliwathibitishia maofisa hao kuwa alifuata taratibu zote katika kupata zabuni na kununua chumvi hiyo aliyoinunua Nakuru nchini Kenya ambapo kabla ya kwenda kununua aliwashirikisha maofisa wa NCAA ambao walimuonyesha aina ya chumvi inayotakiwa.

Sampuli ya chumvi hiyo ilipelekwa kwanza katika Maabara ya Mifugo, Temeke, Dar es Salaam, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na baadaye Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Majibu ya vipimo ya chumvi hiyo yameanza kutoka na maabara ya mifugo imethibitisha chumvi hiyo kuwa na chembechembe za mawe ambayo yanaweza kuleta athari kwa mifugo. Hapa ndipo ninaposema maofisa wote wa NCAA waliohusika katika mchakato wa kuingiza chumvi hiyo, wachukuliwe hatua.

Nasema wachukuliwe hatua kwa sababu wafugaji katika bonde la Ngorongoro hawana imani kabisa tena na NCAA na wafugaji wanajenga hoja kuwa huenda kuna mpango wa kutaka kuua mifugo yao.

Wafugaji pia wanadai tofauti na miaka yote, walikuwa wakishirikishwa katika mchakato wa kutafuta mzabuni wa kununua chumvi hiyo lakini safari hii hawakushirikishwa jambo ambalo linazua sintofahamu.

Kutokana na malalamiko hayo ya wafugaji, kuna umuhimu kwa serikali hususani Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kufutilia kwa karibu jambo hili ili wale wote waliohusika katika kuingiza na kusambaza chumvi hiyo waweze kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Ni wazi kuwa kwa muda mrefu uhusiano kati ya wafugaji na NCAA hauko vizuri kwa kuwa wafugaji wanaamini kuwa mamlaka ina ajenda ya siri na mifugo yao. Wakati sasa umefika katika kujenga mahusiano mazuri kati ya wafugaji na mamlaka, zianze kipindi hiki kwa kuwachukulia hatua maofisa waliohusika katika ununuzi wa chumvi hiyo.

## DARASA LA NDOA

# 2022 UWE MWAKA WA MABADILIKO KWA KINABABA MALEZI YA FAMILIA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

TUMEUANZA mwaka 2022 na takriban tunafikisha siku 10 tangu tulipopata neema ya kuuona. Kwa mtazamo wangu, ni mwaka ambao kinababa tunapaswa kuonyesha kwa vitendo nafasi zetu kama kichwa cha familia.

Kimsingi, baba ni msingi wa familia. Uwapo wa baba katika familia ni muhimu kwa kuwa ndiye mbeba maono na mwekezaji wa misingi ya nidhamu na ustawi wa familia yake. Baba anapotimiza majukumu yake, anaweka misingi imara ya nidhamu, heshima, ustawi na maadili mema.

Maandiko Matakatifu ya Mungu yanaainisha nafasi na wajibu wa baba katika familia. Jukumu la msingi alilopewa baba ni kutunza na kuwa kiongozi wa familia yake (most sacred responsibility). kinababa wanategemewa kuwa na uwezo wa kuongoza na kutunza familia zao.

Nidhamu, heshima, ustawi na maadili mema hujengwa pale baba anapompenda mke wake, anaposikiliza watoto wake, anapowatunza, anapowafunza, anapowaonya, anapowarekebisha, anapowaadabisha. Hapo anapoweka kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia familia ili kujenga familia imara. Baba anapotimiza majukumu yake anaongeza na kutunza thamani, mamlaka, na nafasi yake kwa familia. Baba anayewajibika na kuwa na muda na familia yake ni uthibitisho dhahiri wa kujali na kutoa kipaumbele kwa wale wa nyumbani mwake.

Katika miaka ya karibuni, tumeanza kuzoea kusikia jamii yetu ya leo ni jamii isiyokuwa na kinababa. Nafasi na maana ya baba inaanza kukosekana na kupotea. Hii ni kwa sababu baadhi ya kinababa kwa kisingizio cha kazi, majukumu na mambo mengine binafsi, wamejitenga na kutelekeza familia zao.

Mamlaka ya kinababa wengi katika jamii ya leo yameanza kutiliwa shaka. Ziko baadhi ya familia ambazo baba awepo au asiwepo, mke na watoto hawaoni tofauti yoyote. Awepo sawa, asiwepo sawa. Hali hii ni hatari kubwa kwa mustakabali wa familia.

Wako baadhi ya kinababa ambao hawawajibiki katika familia zao (irresponsible fathers) na wamebaki na sifa ya kuwa mwanamume mashine na kupoteza sifa na maana halisi ya kuwa baba. Kimsingi, kinachomfanya mwanamume aitwe baba si maumbile yake bali majukumu aliyoyabeba kwa ajili ya familia yake, hivyo baba asiyewajibika na anayetelekeza familia yake ni muuaji na anapoteza sifa ya kuitwa baba.

Mwenyezi Mungu amemweka baba katika familia ili kupitia heshima, hadhi na utambulisho wake kama mwanamume, awajibike, awe karibu na watoto na mke wake na kushirikiana naye kila kitu, furaha na huzuni, matumaini na changamoto zingine. Wako kinamama wameolewa lakini maisha wanayoishi hayana tofauti na wale wasio na waume (single Mothers).

Inafaa baba aitunze familia yake, awepo na kupatikana kwa ajili ya mke wake na makuzi ya watoto. Baba asiyekuwa na muda na familia yake, anapoteza thamani na umuhimu wa uwapo wake. Uwapo wake unakuwa hauna mguso (impact) kwa mke wake na watoto kwa sababu hapatikani nyumbani.

Familia nyingi zimekosa kufurahia uwapo wa baba kwa sababu muda mwingi baba hapatikani nyumbani. Katika hali isiyotarajiwa, unakuta mke anapoteza hisia (feelings) na mvuto dhidi ya mume wake. Watoto nao wanapoteza pendo kwa baba yao. Wanamwona baba yao ni mtu mkatili asiye na upendo. Hali hii imesababisha watoto wengine wakiwa watu wazima, thamani na umuhimu wanaelekeza kwa mama zao zaidi kuliko baba zao kwa sababu mama ndiye aliyekuwa na muda nao.

Kinababa wengi wakiishia kuleta mahitaji ya nyumbani wanaona wamemaliza. Wanasahau kwamba kutunza familia ni zaidi ya kutoa mahitaji ya nyumbani. Familia inamhitaji baba zaidi kuliko vitu au mahitaji wanayopewa. Ukaribu wa baba kwa familia yake ni muhimu sana. Baba anapokuwa na muda na familia yake, mke na watoto wanajisikia kuwa salama na kupendwa. Kwa mantiki hii, thamani na umuhimu wa uwapo wa baba katika familia yake unaongezeka.

Pamoja na majukumu mengi tuliyo nayo kinababa, ni muhimu kutengeneza muda wa kuwa na familia. Ni muhimu kufanyakazi kwa ajili ya maisha lakini tunahitaji muda wa kazi na muda wa familia (work is important, so is your family). Kazi isiwe kisingizio cha kudumu cha kukosa muda na familia. Baba asiyetengeneza muda wa kuwa na familia yake anatengeneza bomu litakalomlipukia, litakalomjeruhi na kumwangamiza wakati wowote.

Kwa upande mwingine, kinamama wanao wajibu wa kutengeneza mazingira ya kuvutia nyumbani ili waume zao waone nyumbani ni mahali pa kuishi na kustarehe. Hii inatokana na ukweli kwamba baadhi ya kinamama wamekuwa sababu ya waume zao kuwa mbali nao kutokana na dharau, ujeuri, ukorofi na maneno yao makali. Kina mama wanao wajibu wa kuhakikisha waume zao wanajisikia ni wafalme (kings) ndani ya nyumba na wao kuwa malkia wa nyumba (queens of the household).

Inapendeza na kutia moyo pale familia inapomfurahia baba na baba anapoifurahia familia yake. Furaha ya familia hualika uwapo wa Mungu na baraka katika familia. Ikumbukwe kwamba baraka au laana kwa yale tunayohangaikia, huanzia katika familia. Kwa hiyo kazi na majukumu visiondoe utu wako na thamani ya familia yako.

Kinababa tubadilike na kuwa viongozi wema wa familia katika Mwaka mpya wa 2022. Hapo ndipo tutaziona baraka na ustawi katika familia zetu, jamii na taifa kwa ujumla.

• Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha

# MAISHA

JANUARI 9, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

## SALAD YA NYAMA YA KUOKA



Ukurasa 15

## NYUMBA:

Zingatia haya unapopanga nyumba




## KATUNI

Ukurasa 16





SUGUA GAGA


# Tunza miguu kwa chumvi, asali

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA










## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
INA, MWA, SAUMU, LAANA, NYUNGU, LAWAMA

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya Adaktari

MTOTO Sara akiwa varandani na mama yake majira ya saa 12:00 jioni, wakitafuna karanga, alimuita mama yake na kumuuliza.

Sara: Mama

Mama Sara: Abee binti yangu

Sara: Naomba nikuulize kitu kuhusu mgaa gaa

Mama Sara: Mgaa gaa ni nani mwanangu

Sara: Simjui anaishi wapi ila mwalimu ndio alitufundisha kumhusu yeye.

Mama Sara: Aliwafundishaje?

Sara: Alitufundisha kuwa huwa hali wali mkavu.

Mama Sara: ilikuwaje akawafundisha hivyo?

Sara: Alisema kuwa eti mgaa gaa na upwa hali wali mkavu.

Mama Sara: aaah kumbe mwanangu, sio hivyo. Ni methali inayosema mgaa gaa na upwa hali wali mkavu, inamaanisha kila anayetoka kutafuta, hakosi riziki.

Sara: hahaha kumbe ndio hivyo mama.

SWALI:
Paa ni jamii ya Mnyama gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mwaka huu 2022 unaona nini mbele yako?

KARIBU tena msomaji katika safu yetu hii tuendelee kutafakari ujio wa mwaka huu mpya. Kila mtu mbaye Mungu amempa kibali cha kuuona, naamini yako mambo mengi anayotarajia kuyaona au kufanya katika maisha yake.

Nami leo nikuulize msomaji wangu, unaona nini mbele yako mwaka huu wa 2022? Mungu akamuuliza Nabii Yeremia, “Unaona nini?” Yeremia akamjibu kile alichokiona Mungu akamwambia, “Umeona vyema”.

Unaweza kuona vitu fulani mwaka huu lakini usione vema. Mungu anaweza akafungua milango ya baraka mbele yako, akafungua fursa mbalimbali mbele yako lakini wewe usizione.

Je, mwaka huu unaona kitu gani? Yuko mtu ukimuuliza swali hili atakuambia, naona kufa kufa hivi au naona kama sitafanikiwa. Watu wengi karibu asilimia 90 hawaoni vema. Wako wanaoona hasara, ugumu, woga au wanaoona mambo mabaya tu.

Hata wakiota ndoto, zinakuwa mbaya. Asilimia kubwa ya watu hawaoni mambo mema bali wanaona yaliyo mabaya. Mungu anaweza kukuonyesha kitu lakini wewe ukasema huu ni mtego, kumbe amekuonyesha kitu kizuri cha kufanya.

Kwa mfano, anaweza akakujia mtu akakuambia, “nimejisikia nikupe mtaji”. Lakini ukawa na shaka yaani huamini kwamba ni jambo jema la kukuvusha kiuchumi.

Anakuja mtu anakushauri kafanye biashara fulani lakini wewe unatilia shaka na kuhoji kwamba pengine ni mtego wa kishetani. Kumbe Mungu hutumia watu kumbariki mtu au hutumia watu kumuinua mtu.

Unaweza kuwa mahali akaja mtu na kuongea kitu cha ajabu ambacho kitamuinua mtu. Au akaja mtu mahali akaongea jambo fulani ambalo ulikuwa hujui, au akaongea mtu kuhusu biashara ambayo hujawahi kuiwaza.

Na wewe pasipo kujua kwamba kumbe ni Mungu anasema nawe kupitia watu wa aina hiyo. Na wewe unabaki kuhoji kwamba mambo hayo ni ya kitapeli au mtego! Mungu anaweza kabisa akafungua mlango wako wa mafanikio au baraka lakini usiuone.

Mungu anaweza kukuletea watu lakini usiwaone au usiwatambue. Je, unaona nini mwaka 2022? Unapouanza mwaka huu vipo vitu unaviona, ipo taswira mbele yako ya vile ungependa vifanyike kwenye maisha yako.

Yamkini yako mambo ungependa yatokee mwezi wa nne au wa sita na kuendelea. Inatakiwa ndani yako uone. Mungu ametoa uchaguzi wa aina mbili kwa wanadamu. Kumchagua yeye anayetaka mema au kumchagua shetani anayetaka mabaya!

Wewe unaona nini kwa maana kwamba unachagua nini mbele yako. Viko vitu mwaka huu unatakiwa uvione kabla ya kutokea. Ulimwengu wa roho hauanzi kitu bali unaanza kukiona.

Kwa mfano, utawaza, mwaka huu naona nafungua ofisi yangu au duka, biashara fulani. Mwaka huu naona nitaenda ulaya, nitajenga nyumba, nitapata mchumba, nitaoa. Yaani unachokiona ndicho utakachokipata. Aidha umeona vizuri au umeona vibaya!

Chochote utakachokiona ndicho utakipata. Ukiona matatizo, nayo yatakupata, ukiona mafanikio utayapata. Mwaka huu yamkini kipo kitu unakiona. Ukiona unainuliwa itakuwa hivyo na ukijiona huinuki, na kweli hutainuka. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Mpenzi msomaji wangu, vile vile ukiona unabarikiwa mwaka huu, hakika ndivyo itakavyokuwa.

Katika hali ya kawaida, mtu huishia alipoona. Huwezi kupata chochote zaidi ya unavyoona. Hata Mungu hawezi kukupa kitu zaidi ya unavyoona.

Pia ni ukweli kwamba mwisho wa kuona kwako ndio mwisho wa utendaji wa Mungu. Watu wengine wamekuwa wakitumia macho ya watu wengine kuendesha maisha yao, jambo ambalo si sahihi.

Ni muhimu mwaka huu watu wajiwekee malengo yatakayowavusha. Kama mwaka jana hukuweza kufanikisha jambo fulani, jiulize ulikwama wapi. Na jiulize je, ulimshirikisha Mungu katika mipango yako?

Kumshirikisha Mungu kuna faida kubwa. Atakuwa ndiye kiongozi na msimamizi mkuu kuratibu mambo yako. Muombe Mungu akupe neema ya kuisikia sauti yake katika kufanikisha mipango yako ya mafanikio.

***Msomaji wangu, bila shaka umejifunza kitu hapo. Niishie hapa kwa leo. Wiki ijayo nitaenda zaidi jinsi baadhi ya watu hutumia macho ya watu wengine katika maisha. Ni kwa namna gani, fuatilia. Je, una maoni? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tumemaliza madarasa sasa ni nyumba za walimu, vitabu na maabara

HII ni wiki ya mwisho ya maandalizi kwa wanafunzi wote kurudi shuleni baada ya likizo ya mwezi mmoja. Wale wanaostahili kupanda kidato au darasa sasa wanaingia hatua mpya ya maisha yao kitaaluma.

Serikali imeeleza kazi kubwa iliyofanyika hasa ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 15,000 kwenye halmashauri zote nchini, ambavyo vitawezesha wanafunzi wote wanaoingia kidato cha kwanza kuingia bila tatizo tofauti na miaka mingine waliyochelewa kuingia kutokana na ukosefu wa vyumba vya madarasa.

Hili limewezekana kutokana na ubunifu uliofanywa na serikali wa kukopa Sh. trilioni 1.2 ambazo pamoja na mambo mengine zimeelekezwa kwenye kuboresha shule za sekondari na msingi, lengo likiwa kumwezesha mtoto wa kitanzania kusoma bila matatizo.

Pia Waziri mwenye dhamana ya tawala za mikoa na serikali za mitaa alisema kuna zaidi ya shule shikizi 3,000 zinaboreshwa maeneo mbalimbali ili kuwasaidia wanaotembea mwendo mrefu kusoma kama wale wanaosoma kwenye shule kuu.

Zote hizi ni jitihada za kuboresha elimu nchini, hivyo sasa tuna miundombinu ya kutosha kwa kuwa mwanzo tulianza na shule za kata ambazo zilisambaa na sasa zimeboreshwa na zingine zimekuwa shule kubwa zinazofanya kazi kubwa ya kunoa bongo za wanafunzi.

Haitarajiwi ifikapo Januari 17, mwaka huu, kuwe na mwanafunzi atakayeshindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya uhaba wa miundombinu bali sasa nguvu kubwa ielekezwe kwenye upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada ili elimu ipatikane.

Liko tatizo kubwa la upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi wa shule za umma kiasi cha wengi kushindwa kusoma baadhi ya vitabu. Badala yake wana hadithiwa na mwalimu wa somo husika na hiyo ndiyo hutumika kujibu mtihani.

Kama tunataka kujenga utamaduni wa kujisomea kama alivyosema Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, wakati akizindua Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, ni lazima kuwa na vitabu vya kutosha shuleni pamoja na maktaba zitakazowawezesha kujisomea.

Jitihada zimefanyika kwa kuwa na maktaba hadi ngazi ya tarafa ambayo itahudumia watu wote,lakini ni lazima maktaba hizo ziwepo kuanzia shule za msingi ili watoto wapende kujisomea na kukua katika hali hiyo ya kuongeza maarifa kupitia vitabu vya masomo na visivyo vya masomo.

Pia ni muhimu kwa sasa kuelekeza nguvu kwenye upatikanaji wa vifaa vya masomo ya sayansi ili wanafunzi wasisome kwa nadharia bali kwa vitendo.

Hadi sasa wanafunzi wengi wa shule za umma wanashindwa kusoma masomo ya sayansi kwa kuwa hakuna vifaa muhimu na walimu wa kutosha. Kama tunataka kuongeza wasomi kwenye eneo hilo, ni lazima nguvu kubwa ielekezwe huko kwa kuwekeza kwenye vifaa vyote muhimu.

Kutokana na ukosefu wa vifaa vya maabara, ilifikia wakati kukawa na mitihani miwili ya nadharia na vitendo. Wale wenye shule iliyokamilika kwa maana ya vifaa vya maabara basi walifanya mitihani yote lakini wengine walifanya nadharia.

Jambo lingine ambalo ni muhimu na msingi wa elimu yetu ni kuwajali walimu kuanzia mahali wanapoishi na familia zao. Hii inawajenga kisaikolojia na kuwaongezea ujasiri na morali ya kazi.

Hivi karibuni iliripotiwa kuna mwalimu anatumia darasa kama nyumba ya kulala. Tufikirie mtu kama huyo ni wakati gani anaifurahia kazi yake ili atimize wajibu wake wa kunoa bongo la mtu ambaye huenda akawa kiongozi wa taifa letu siku zijazo.

Naelewa kuwa mambo ni mengi na changamoto ni nyingi lakini pia kukosekana kwa utayari wa watendaji kuhakikisha kila shilingi ya umma inakwenda kufanya kazi sahihi lakini hali inakuwa tofauti kwa kuwa wakati mwingine fedha inaishia mikononi mwa wachache na miundombinu inajengwa chini ya kiwango.

Ni muhimu kuboresha au kujenga miundombinu ili walimu wasipate shida,nina hakika wakiwa na uhakika wa kuishi wao na familia zao watazidisha kuipenda kazi pamoja na ubunifu utakaoboresha kiwango cha ufahulu.

Naamini tutafika wakati hatuzungumzii miundombinu mipya bali kuboresha iliyopo na kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi, kwa kuwa kila shule itakuwa imejitosheleza kwa walimu, miundombinu na vitabu vyote muhimu.

Haya yote ili yafanikiwe ni lazima ushiriki na utayari wa jamii uwepo kupitia kamati za shule huku wakizingatia sheria na kanuni kwa kuwa ziko baadhi ya kamati zimepitisha michango iliyozua manung'uniko ambayo imeanza kutekelezwa na walimu wakuu na wakuu wa shule, huku wazazi wakilalamika na ofisa elimu hajui lolote.

Lazima kuzielimisha kamati za shule ili zijue wajibu na mipaka yake ili kuepusha walimu wakuu na wakuu wa shule kuingia matatizoni kwa kutekeleza kilichoshauriwa na kamati kama ilivyotokea Tarime ambako kuna shule inayotoza Sh. 5,000 kwa kila mwanafunzi anayeandikishwa.

***Mungu ibariki Tanzania.***











Tarehe 31/10/ 2021 ilikuwa ni siku ya furaha na shangwe kwa John Mlay alipofunga ndoa takatifu na Lauindeni Kisanga, katika Kanisa Katoliki Mwenyeheri Anuarite, Parokia ya Makuburi, baadae tafrija fupi iliyofanyika katika ukumbi wa Mwika Social Hall mkoani Dar es Salaam.

MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# EPUKA MAVAZI HAYA
# UKIALIKWA KWENYE HARUSI

MWAKA mpya umeanza kwa kasi, watu wanajiandaa kufanya sherehe mbalimbali.

Moja ya sherehe muhimu ambazo watu hupenda kuhudhuria ni harusi, hivyo lazima uwe tofauti mwaka huu pale unapopata mwaliko kama ndugu, jamaa au rafiki.

Katika sherehe hizo za kipekee katika jamii zetu, ni muhimu kuzingatia makosa utakayofanya na kuharibu mwonekano wako.

Kutokana na muktadha huo, nitawaeleza vitu vya kuzingatia kabla hujaamua kuvaa nguo ambayo utatoka nayo kwenda harusini.

**USIFANYE MAKOSA HAYA**

Usivae nguo nyeupe , kwani rangi nyeupe hutumika sana na maharusi kwenye sherehe zao.

Kama huna hakika na rangi, angalau valia nguo ya rangi ya maziwa, kijani au bluu ili kukufanya uwe wa kipekee.

Usithubutu kuvaa viatu vya visigino virefu ambavyo huwezi kuvimudu kutembea, hakikisha unavaa vile unavyoona unaweza kutembea kwa madaha na tabasamu pana.

Usivae mavazi yanayo acha sehemu kubwa ya mwili wako wazi, hata kama nguo imekupendeza sana iache kuepuka kuwa gumzo katika sherehe ya watu.


Hakikisha unapo jiangalia kwenye kioo, jaribu kuangalia jinsi utakavyo kaa na kuinuka kwenye kiti chako na uone kama vazi hili litakufaa.

Kama unapenda kuvaa suruali, basi vaa 'jamp suti' yaani suruali yenye upana kiasi na koti la kupendeza.

UREMBO

**Na Mary Geofrey**







SUGUA GAGA

# Tunza miguu kwa chumvi, asali

MIGUU ni sehemu ya viungo vya mwili inayochangia urembo wa mwanamke.

Kwa ujumla miguu yenye ngozi laini na rangi asilia humfanya mtu kujiamini na kuwa na furaha kila wakati.

Baadhi ya wanawake wana matatizo sugu ya kuwa na nyayo ngumu zilizokatika inayojulikana kama magaga.

Tatizo hilo linatokana na kutofahamu namna nzuri ya kuitunza na kuendelea kubaki katika umaridadi wake wa utotoni.

**Njia za kuosha miguu**

Chukua maji ya uvuguvugu changanya na chumvi, kisha loweka miguu yako kwa dakika tano kabla ya kuisafisha.

Kisha safisha kwa kusugua hakikisha mabaki ya ngozi yanaisha katika miguu.

Weka maji changanya na asali, kisha lowesha miguu yako hii husaidia kulainisha unyayo wako pamoja na kuondoa michubuko iliyopo katika unyayo.

Futa miguu yako kwa kitambaa safi kuanzia vidole vyako mpaka unyayo wako.

Usipokausha vema hupelekea kupata fangasi na kupelekea miguu kunuka unapovaa viatu vya kufunika.

Pendelea kutumia mafuta ya watoto kujipaka katika unyayo wako au paka glyceline kisha vaa soksi wakati wa kulala hii husaidia kulainisha unyayo.

Ongeza kiwango cha kunywa maji angalau lita moja kwa siku ambayo husaidia ngozi yako kuendelea kuwa nyororo.

Mwisho

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# SALAD YA NYAMA YA KUOKA







WENGI wetu tunapenda kula salad kama chakula ili kuzuia kuongeza uzito. Haya mapishi yanaonyesha jinsi ya kuongeza vionjo kwenye salad kwa kula na nyama ya kuoka.

Nyama iliyookwa ni afya na nzuri zaidi kula kwa kiasi na kwa hamu.

**MAHITAJI**

Nyama nusu kilo ya mbuzi au ng'ombe, karoti mbili kata vipande vidogo, tangawizi moja.

Vitunguu saumu viwili, pilipili hoho mbili ya kijani na nyekundu, kitunguu maji kikubwa kimoja kikatwe vipande vidogo na salad.

Nyanya mbili, pilipili manga, olive oil, limao moja lililokamuliwa na tango moja.

Namna ya kuandaa

Pasha moto oven kwenye nyuzi 250 na acha iwe ya moto kwa muda wa dakika 5 hadi 10.

Andaa nyama, kata vipande wastani, osha kisha weka kwenye bakuli ya kioo au chombo unachotumia kupikia kwenye oven.

Ongeza viungo, kitunguu saumu, tangawizi, pilipili manga na changanya vizuri.

Weka chumvi, changanya vizuri na kamulia limao, kisha changanya vizuri mchanganyiko.

Menya viazi, kata vipande. Changanya kwenye nyama.

Weka karoti, pilipili hoho, kitunguu maji na changanya vizuri, weka olive oil, changanya vizuri.

Weka mchanganyiko wa nyama na viungo kwenye oven na weka kwa muda wa dakika 40.

Angalia mara kwa mara kama nyama inaiva vizuri au inaungua, na geuza ili kuifanya iive kwa uwiano mzuri.

**ANDAA SALADI**

Osha saladi yako vizuri, weka kwenye chombo kikubwa, kata kwenye vipande vidogo kwa kutumia mikono, kata nyanya, tango kwenye vipande vidogo, changanya salad, nyanya na tango.

Baada ya nyama kuiva, changanya kwenye sahani yenye salad na itakuwa tayari kwa kuliwa wakati wowote.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# ZINGATIA HAYA UNAPOPANGA NYUMBA

MSIMU umewadia wa mwanzo mwa mwaka, kipindi ambacho watu wengi hupendelea kutafuta makazi kwa ajili ya kuishi.

Ni vyema katika kipindi hiki kuwa makini zaidi katika kutafuta nyumba ambayo haitakuletea shida, hakikisha hukurupuki.

Hakikisha unazingatia mambo muhimu kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho wa kupanga nyumba kwa ajili ya kuishi.

Moja ya mambo hayo ya kuangalia ni mahali nyumba ilipo na umbali. Kumbuka kuna uwezekano mkubwa ukaona nyumba nzuri kwa mwonekano na ukatamani upange kwa ajili ya kuishi lakini ikawa iko mbali zaidi au ikakulazimu kutumia pesa zaidi kwa upande wa usafiri.

Endapo unatumia usafiri wa umma, itakulazimu kila ukifika kituoni lazima utumie tena usafiri mwingine ambao nao ni gharama kubwa kufika kwenye nyumba hiyo, hivyo ni lazima ufikirie kwa makini kufikia uamuzi wa kuishi kwenye nyumba hiyo. La sivyo unaweza ukashindwa kuweka akiba kwa ajili ya kufanyia maendeleo mengine.

Jambo lingine la muhimu la kuangalia kabla ya kupanga nyumba ni kuangalia kama nyumba hiyo itahitaji marekebisho makubwa.

Kuna baadhi ya nyumba zinakuwazinaonekana vizuri kwa nje lakini ndani zinahitaji marekebisho makubwa ambayo huenda yakakuongezea gharama kubwa ambazo hukutegemea.

Kwa mantiki hiyo, inabidi ujiulize kama kuna ulazima wa kuishi kwenye nyumba hiyo au kama unaweza kutafuta nyingine na ukaepuka hayo isipokuwa tu kama mmiliki yuko tayari kurekebisha kwa gharama zake.

Lingine ni masharti yanayokuwa yamewekwa kwenye nyumba husika. Baadhi ya wenye nyumba huweka masharti magumu na wakati mwingine mpangaji anapofika kuhitaji nyumba hawasemi ukweli na badala yake baada ya kulipia na kuanza kuishi, ndipo huanza kuyasema kidogo kidogo kwa wapangaji. Kwa hiyo ni vyema kudodosa hilo kabla ya kufikia uamuzi wowote.

Hakikisha unausoma kwa makini mkataba kabla ya kulipia pesa yako kwenye nyumba. Wengi hufikiri ukishalipa kodi basi hakuna jambo la kwenda vibaya lakini mambo yanaweza kubadilika.

Kama ambavyo unakubali kwa kuandika kwamba utalipa kodi kwa wakati na kuitunza vyema, hakikisha pia na mkataba wako unausoma vizuri na kama kuna mambo ambayo mwenye nyumba anapaswa kuyatekeleza afanye hivyo, kama ilivyo kwako na ukibaini kama kuna kitu kinakufunga ni bora uulize kabla ya kuingia rasmi kwenye nyumba.

Pia huu ni msimu wa mvua, hivyo hakikisha unazingatia endapo eneo nyumba iliyopo hapajai maji kwa sababu hilo nalo ni tatizo lingine linaloweza kukuletea shida.



## Jinsi ya kupamba ukuta kwenye ukumbi juu ya sofa




MABANGO na picha hutumiwa mara nyingi katika mambo ya ndani ya sebule. Mapambo haya yanaweza kutumika katika mpango wowote wa rangi na mtindo, ambao hautabadilisha tu chumba hiki, lakini pia utoe maoni ya kupendeza kwa wageni wa nyumba hiyo.

Ikiwa kuna vitu vingi, basi ni bora kuziweka picha kwa umbali wa sentimeta 5 hadi 15 kutoka kwa kila moja, katika namna hii mapambo haya yatatambuliwa kama kitu kimoja.

1. Kuna vifaa vingi vya kumaliza ambavyo vinaweza kupamba na kutoa uhalisi kama ramani ya kijiografia ya kisasa au ya zamani, bidhaa za kughushi, mapambo ya mada, saa, kioo, sahani na mengine zaidi.
2. Kama mapambo ya chumba katika mtindo wa mavuno, meza ya mapambo inafaa. Katika mambo ya ndani ya kisasa, medali za polyurethane zilizotawanyika kwa nasibu kwenye ukuta zitakuwa sehemu ya uchezaji.
3. Ikiwa chumba kimepambwa kwa mtindo fulani, basi mapambo pia yanaweza kuwekwa ukutani. Kwa mfano, usukani au nanga itafaa mtindo wa baharini, ambao utakuwa kituo cha umakini. Kuna njia zingine:
4. Ili kufanya sebule iwe ya kupendeza zaidi, pamba ukuta, juu ya sofa na rafu. Juu yake unaweza kuweka sio vitabu tu, bali pia vifaa vingine kama sanamu, zawadi na picha.

## KATUNI


JUKWAANI
KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
'NILIKUTEST TU' WALA SINA KIU NISHA-IMALIZIA KWA WANAO-JUA INAVYOKATWA
HATA MIMI NIMEKONGA KIU YANGU NINA MTAALAM!
"UKATA"
2022
DEREVA KAMA WEWE UNATAKA KUJITOA ROHO KWA STRESS ZA ADA TUSHUSHE NENDA UKAFE PEKE YAKO!
UNAJUA DEREVA NIKI-KUANGALIA MACHONI SIONI DALILI ZA WEWE KUENDELEA KUISHI!
UKIWEZA DROPU
BADALA YA KUMLAZIMISHA ASIMAMISHE GARI ETI TUNADISKASI
NIKUMBUSHE MWAKA JANA ULICHONIAHIDI
NILIKUAHIDI 'AHADI' YA KUKUAHIDI
HIVI NANI ALIWEKA UTARATIBU WA 'JANUARI KUWA DUME?' HADI KIWESE SINA!
BOSI LEO UKIRUDI NA POMBE ZAKO UWE NA ADABU!
NDIO MAANA NIMEKUPA HIYO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MWACHE MKEO UMJUE MWIZI WAKO

HABARI KIMATAIFA

# Sheria za COVID-19 zapigiliwa msumari kwenye baa, migahawa, Ujerumani

**BERLIN,** UJERUMANI

WATEJA kwenye baa na migahawa kote nchini Ujerumani, watalazimika kuthibitisha kuwa wamepata dozi ya tatu ya chanjo au waonyeshe cheti cha vipimo kuthibitisha kuwa hawajaambukizwa ndipo waruhusiwe kuhudumiwa.

Masharti hayo mapya yamejiri baada ya mkutano wa Ijumaa, kati ya Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz na wakuu wa majimbo yote 16.

Akiyatetea masharti hayo, Scholz alisema anafahamu ni magumu lakini yanahitajika ili kusaidia kuzuia au kudhibiti maambukizi hata katika siku za baadae kuliko jinsi hali ilivyo kwa sasa.

Scholz alisisitiza umuhimu wa kupata dozi ya tatu ya chanjo ambayo ni nyongeza, akisema ndio kinga bora zaidi dhidi ya aina ya kirusi cha Omicron.

Scholz pia alifupisha muda ambao watu watahitajika kukaa karantini kutoka siku 14 hadi siku 10. Muda huo huweza kufupishwa hata zaidi ikiwa mtu haonyeshi dalili ya kuambukizwa na vipimo pia vithibitishe kuwa hajaambukizwa.

Wafanyakazi katika sekta muhimu zaidi mathalan wahudumu wa afya, maofisa wa polisi na watoa huduma za dharura wataruhusiwa kukaa karantini hata siku chache zaidi.

**Waiochanja kuendelea kukabiliwa na vikwazo**

Kulingana na masharti hayo mapya, watu ambao wameshapata dozi ya tatu ya chanjo hawatahitajika kukaa karantini hata wakijumuika na mtu yeyote aliyeambukizwa COVID-19.

Sheria inayosisitiza kuwa watu 10 pekee ndio wanaruhusiwa kujumuika pamoja ikiwa wamechanjwa au wamepona COVID-19, itaendelea kutekelezwa.

Wale ambao hawajachanjwa wataendelea kukabiliwa na vikwazo vikali zaidi.

Mkutano huo wa kwanza wa Olaf na wakuu wa majimbo katika mwaka 2022, ulijiri wakati serikali ya Ujerumani ikiimarisha kampeni ya chanjo ili kukabili ongezeko la maambukizi kutokana na kirusi cha Omicron.Kwa sasa kampeni ya upokeaji chanjo nchini Ujerumani inazidi kushika kasi, baada ya Sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya.

Hadi sasa asilimia 71 ya watu Ujerumani wameshapokea dozi mbili za chanjo.

Idadi ya watu waliochanjwa dhidi ya COVID nchini Ujerumani ni asilimia 71.5. Aidha asilimia 40.9 tayari wamepokea dozi ya tatu ya chanjo.

Hata hivyo idadi hiyo ni chini ikilinganishwa na hali ilivyo katika mataifa mengine ya Ulaya.

Serikali ya Scholz imejiwekea lengo la kuwachanja watu milioni 30 ili kuhakikisha asilimia 80 ya idadi ya watu wamepokea chanjo ifikapo mwisho wa mwezi huu.

Mnamo Alhamisi, Ujerumani ilirekodi maambukizi mapya 64,340 ya virusi vya Corona. Hii ni kwa mujibu wa taasisi ya Ujerumani inayopambana na maradhi ya kuambukiza Robert Koch.

Idadi ya vifo pia iliongezeka kwa watu 443 hivyo kusababisha idadi jumla ya watu waliokufa Ujerumani kutokana na janga la COVID-19 kufikia 113, 368.



Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz (kushoto) alipokutana na wakuu wa majimbo 16 ya Ujerumani mjini Berlin, kuhusu sheria mpya za kudhibiti maambukizi ya COVID-19

# Wauaji wa Ahmaud Arbery wahukumiwa jela maisha

**WASHINGTON D.C,** MAREKANI

WANAUME watatu wazungu nchini Marekani, wamehukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kumuua Mmarekani mweusi Ahmaud Arbery aliyeuawa mwezi Februari mwaka 2020 akiwa na umri wa miaka 25.

Mahakama ya jimbo la Georgia iliwakuta na hatia Gerg McMichael na mtoto wake wa kiume Travis McMichael na jaji aliwapa kifungo kisichokuwa na uwezekano wa kusamehewa.

William Bryan ambaye ni jirani ya waliohukumiwa mwanzo, ambaye alipiga picha ya video ya tukio la kuuawa kwa Arbery pia alihukumiwa kifungo cha maisha jela, lakini hukumu yake inampa uwezekano wa kusamehewa.

Akitoa hukumu yake, Jaji Timothy Walmsley alisema hukumu hizo, zinawawajibisha wahukumiwa kutokana na mauaji yao ya kinyama.

Kifo cha Arbery kilitokea alipokuwa akifanya mazoezi, pale alipofukuzwa na watu watatu na kumuua.

Video ya kuuawa kwake ilisambaa katika mitandao ya kijamii na kuzusha ghadhabu na shutuma nchini Marekani na ulimwenguni kote.

Kifo chake kilitokea miezi mitatu tu kabla ya kuuawa kwa Mmarekani mwingine mweusi George Floyd, ambaye kifo chake pia kilizusha ghadhabu na maandamano ulimwenguni kote.

## Ethiopia yamuachia huru kiongozi wa upinzani na wengine

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

CHAMA cha upinzani nchini Ethiopia cha Balderas kwa demokrasia halisi, kimesema kiongozi wake Eskinder Nega, ameachiwa huru kutoka gerezani baada ya kusota jela kwa mwaka mmoja na nusu.

Kituo cha televisheni kinachomilikiwa na serikali ya Ethiopia kimetangaza kuwa, kiongozi mwingine wa upinzani kutoka jamii ya Oromo, Bekele Garba, pamoja na Jawar Mohammed ambaye ni mwanasiasa na mmiliki wa chombo cha habari pia wameachiwa huru.

Eskinder aliyekianzisha chama cha Balderas alikamatwa mwaka 2020 kufuatia machafuko yaliyozuka kutokana na kuuawa kwa mwanamuziki na pia mwanaharakati Hachalu Hundessa.

Eskinder alishtakiwa mwezi Septemba mwaka 2020, kwa madai ya ugaidi katika mahakama kuu nchini Ethiopia.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres alikaribisha hatua ya kuachiwa huru kwa Eskinder.

Alisema anatumai juhudi za kuwezesha misaada ya kiutu kufikia maeneo ambayo yameathiriwa kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo zitaimarishwa.

Vikosi vya serikali ya Ethiopia vimekuwa vikipambana na waasi katika jimbo la Tigray kwa muda wa mwaka mmoja sasa.

Katika wiki za hivi karibuni, Waziri Mkuu wa nchi hiyo Abiy Ahmed, alisema nchi yake inahitaji mchakato wa maridhiano ya kitaifa.

## Mawaziri wa NATO waandaa mkutano kuhusu mzozo wa Urusi, Ukraine

**MOSCOW,** URUSI

MAWAZIRI wa Mambo ya Nje wa Jumuiya ya Kujihami ya NATO, juzi walifanya mkutano kujadili hatua ya Urusi kuwarundika wanajeshi wake katika mpaka wake na Ukraine.

Kwenye mkutano huo uliofanyika kwa njia ya video, Katibu Mkuu wa NATO Jens Stoltenberg, alisisitiza kuwa muungano huo wa kijeshi unaiunga mkono Ukraine ambayo hata hivyo si mwanachama wa NATO.

Stoltenberg alisema NATO iko tayari kwa mazungumzo na Urusi kuhusu udhibiti wa silaha.

Aliongeza kuwa Urusi bado inaendelea kuwarundika wanajeshi katika mpaka huo na kwamba kitisho cha kutokea mzozo ni dhahiri.

Mwezi uliopita, Urusi iliainisha orodha ya matakwa yake kwa NATO na Marekani, ikiwa ni pamoja na NATO kuacha kuwapeleka wanajeshi wake upande wa mashariki wa muungano huo.

Rais wa Urusi Vladimir Putin alisema Ukraine kujiunga na NATO itakuwa sawa na kile alichokitaja kuwa kuvuka 'mstari mwekundu'.

NATO ilisema matakwa ya Urusi hayakubaliki, na imesisitiza kuwa Urusi haiwezi ikachagua nani anajiunga au hajiungi na NATO.

## MAKALA

# PENGINE YANATAKA KUTIMIA



Na Magabilo Masambu

KATIKA kabila letu tunako kautamaduni, nafikiri ni kazuri japo pengine kwa maisha ya sasa, inawezekana kasiwe kazuri kulingana na mambo kubadilika hasa katika jamii inayodhani imeendelea.

Kautamaduni kenyewe ni kwamba inapotokea umetembelewa na mgeni kwenye familia yako, ni marufuku kumuuliza kama amekula au hajala na wala huwa mgeni haulizwi kama apikiwe au asipikiwe.

Tunachokifanya mgeni akifika nyumbani, huwa kiti chake kinawekwa mbali na eneo la kuandalia chakula kwa maana ya jiko. Sababu yake ni kwamba hatakiwi kuona wala kujua kama chakula kinaandaliwa kwa ajili yake. Kama atachinjiwa kuku basi kuku huyo huwa hakimbizwi. Yanaweza kutumika mahindi kumkamatisha kimyakimya ili mgeni asisikie kwamba anataka kuchinjiwa kuku.

Sababu kubwa ya kutohitaji asisikie wala ajue kwamba chakula kinaandaliwa kwa ajili yake ni kwamba anaweza kukataa chakula kisiandaliwe kwa madai kwamba ameshakula kumbe ana njaa. Sababu za kukataa wengine huwa wanaona kama wanaleta usumbufu kwenye familia ile na wakati mwingine anaweza kuwaza juu ya bajeti ya familia. Hii ilikuwa inafanyika hivyo kwa sababu hatukuwa na utamaduni pia wa kutoa taarifa kwenye familia yenyewe kwamba nakuja huko au kwa sababu ya kutokuwa na mawasiliano au utamaduni tu.

Ninachotaka kusema wakati mwingine kwenye maisha huwa tunavumilia mengi ndani huku nje tukiendelea kuonyesha tu kwamba mambo ni safi na kwamba hakuna tatizo lolote. Tunatofautiana. Wako wanaoweza kukaa nayo lakini wengine si rahisi kuweka kifuani wanapoona mambo yamewazidia husema hadharani.

Utafiti mbalimbali unaonyesha sababu mojawapo inayotufanya wanaume tufe mapema zaidi kuliko wanawake. Ukiondoa sababu za kibaolojia ni kukaa na mambo mengi kifuani ili kuonyesha uanaume wetu.

Wanaume huwa si wepesi kuonyesha kwamba tumekerwa na hili au lile bali huwa tunataka kumaliza mambo kimyakimya huku yakitumaliza wenyewe kimyakimya mwisho wa siku mengine tunaondoka nayo bila kuyaweka wazi, jambo ambalo ni nadra sana kwa wanawake. Wao huwa wakiona mambo yamewazidi, huweka wazi ndiyo nafuu ya mioyo yao. Hatuna cha kuwalaumu kwani ni asili.

Jambo la pekee tulilo nalo binadamu ni kutoamini pale mambo yanapokaribia ukingoni. Tumejengewa kibri cha kutoamini kama mwisho ndio huu au unakaribia au umefika. Ni mpaka tushuhudie kwa macho yetu kwa sababu tuna asili ya ubishi na kiburi ambacho pengine huwa naamini ndiyo dhambi ya asili yenyewe.

Ukisoma maandiko matakatifu inaonyesha kwamba hata Mungu alipokaribia kuziangamiza Sodoma na Gomola, watu wake walifanywa kuwa na mioyo migumu kiasi cha kutoamini kirahisi jambo kama hilo linaweza kutokea, hivyo waliendelea kutenda maovu mpaka siku walipoona moto unawaka.

Ujenzi wa safina ya Nuhu vivyo hivyo. Mungu alipomwambia Nuhu ajenge safina na kwamba baada ya hapo ataiangamiza nchi kwa gharika, hakuna aliyeamini kwamba inawezekana, hivyo ushiriki katika ujenzi wa safina ukafanywa na Nuhu pekee. Wengine wakaendelea kuwa na mioyo migumu mpaka walipoona gharika inasomba kila kilichoko kwenye nchi.

Ndivyo ilivyo kwetu sisi binadamu wa kileo. Ukiwa unapita njia fulani ukiambiwa huko usipite kuna hatari, hapo sasa ndiyo unataka ukaione hiyo hatari yenyewe kwa sababu tuna mioyo migumu na asili ya kupingana na ukweli (the law of inertia).

Tukitizama, kusoma na kufuatilia historia ya vyama vingi vikongwe barani Afrika, ambavyo vilijiita vyama vya ukombozi, vingi vimejifia jambo ambalo pia mpaka wakati vinakufa au kusambaratika hakuna aliyekuwa anaamini kama inaweza kutokea. Bado wengi wao walijawa na viburi vya utawala na kwamba siku chama hiki kikifa nchi itaingia kwenye matatizo lakini wakashangaa chama kimekufa na nchi iko salama.

Tumeanza kuona moshi mkubwa unafuka nyumbani kuashiria ugali unakaribia kuiva. Wengi wetu bado tuna imani kubwa kwamba haitaweza kutokea. Lakini maandiko yanasema kwamba myaonapo haya ni utungu tu mwisho waja maana yake mwisho unaweza usiwe mbali kulingana na namna mambo yanavyoweza kushughulikiwa au yanavyoweza kupuuziwa kwa sababu ya kibri cha madaraka na utawala.

Inawezekana isiwe leo ikawa kesho tutalaumiana, tutagombana, tutashughulikiana lakini kama mwisho umefika, hayo yote hayatazuilika bali kama yamepangwa kutimia yatakuwa. Baada ya hapo tunaweza kujilaumu kwa jinsi tulivyochukuliana, tulivyofarakana na kadhalika. Ninachoamini hakuna jambo linaweza kutokea bila sababu. Sababu zake huwa zinakuja kujulikana baada ya jambo lenyewe na ndipo kila mtu atakubaliana na hali.

Ushauri wangu tutulie. Kushambuliana wazi hakukuwahi kuleta amani. Unaweza kumwona adui mmoja amesimama mahali pa wazi, kumbe kuna maadui 100 wako vichakani huku wakipiga makofi na shangwe wakati wa mchana na usiku wanageuka na kuwa mizuka.

Inahitajika subira, busara, hekima na uvumilivu wa hali ya juu si katika kushughulikiana bali kutafuta suluhu ya kile kinachotufarakanisha. Kutua kwa mzigo kunaweza kusiwe mwisho wa safari bali kikawa kituo cha kuvuta pumzi ili kufikisha mzigo nyumbani.

Uhakika nilio nao ni kuwa ikiwa tutashindwa kutafuta njia iliyo bora kushughulikia tatizo lenyewe, basi tutakuwa tumetafuta njia rahisi ya kukuza mgawanyiko na mpasuko wa wazi zaidi na mwisho yale yaliyotabiriwa yatatimia hata kama hatuamini.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Watunzi wa dansi walivyomtumia Marehemu Shaaban Robert



Na Adam Fungamwango

TUMEZISIKIA nyimbo nyingi za zamani ambazo tunzi zake zilikuwa na maneno murua, mashairi, fasihi na misemo mbalimbali. Pamoja na kwamba wanamuziki wa zamani walikuwa 'vichwa', yaani walikuwa na akili nyingi katika kutafuta maneno ya kupeleka kwenye hadhara pia wanaonekana walikuwa wanachota maneno kutoka kwenye vitabu vya waandishi mashuhuri wakati huo kama Shaaban Robert na Akilimali Snow-White.

.Zamani watu wengi walikuwa na tabia ya kusoma vitabu mbalimbali vya riwaya na vya mashairi kama ya kina Mathias Mnyampala, Sheikh Amri Abeid Kaluta, Saadan Abdul Kandoro, Akilimali na Shaaban Robert.

Hata wanamuziki pamoja na kutunga nyimbo zao, walionekana kuchota baadhi ya maneno kutoka kwenye vitabu vya waandishi hao wa riwaya na mashairi.

Katika utafiti wangu mdogo nimegundua baadhi ya nyimbo ambazo maneno au vipande vya mashairi vimechotwa kutoka kwenye vitabu mbalimbali vya malenga hao. Wimbo wa Orchestra Safari Sound ya mtindo wa Dukuduku waliimba wimbo mmoja uitwao 'Gaba'.

Moja ya mashairi ya wimbo huo yanasema. "Nimechoshwa eee, nimechoshwa na vituko vyako, afadhali eee, tuachane kwa usalama..."

Kipande cha maneno kimetolewa kwenye shairi la Akilimali, kwenye kitabu chake cha Diwani ya Akilimali. Shairi linaitwa 'Eenenda Mwana Kunenda, nalo linasema hivi.

"Nimechoshwa na vituko, daima vinanikifu, moyo sina pumziko, bali mwingi usumbufu, Eenenda ondoka zako, moyoni unanikifu."

DDC Mlimani Park Orchestra nao walikwenda kuchota kipande cha shairi 'Usiponipenda wewe, wengine watanipenda'. Sehemu ya shairi hilo inasema: "Kama mapenzi yaua, kheri potelea mbali, na kama ni kuugua, nitapona siku mbili, enenda nitapumua na kubwa sumbuko hili."

Mlimani Park, maarufu kama Sikinde, wakachukua kipande kisemacho "Kama mapenzi yaua, kufa sioni muhali."

Kwenye kitabu hicho cha Diwani ya Akilimali kuna shairi lingine liitwalo 'Dunia Rangi Rangile'. Kuna kipande kimoja cha shairi kimendikwa hivi. "Dunia kwa mwanaume, yataka kujichumia, kila pembe na ujitume, nawe kujisaidia, siyo ungoje wachume, ukalie kutumia."

Kwa wale mashabiki wa muziki, wanaweza kujua kabisa kuwa ni bendi gani imetumia kipande hicho cha shairi kukiweka kwenye wimbo wao. Ni Bima Lee ambayo walifanya hivyo kwenye wimbo wao wa 'Masimango'. Wao waliimba hivi. "Sheria ya binadamu yataka kujichumia, kwa jasho lako, kila pembe na ujitume, siyo ungoje kuchumiwa, wewe ukae kutumia bwana eee."

Akilimali Snow-White, ndiye mwandishi ambaye mashairi yake kwa kiasi kikubwa yamechukuliwa na watunzi wengi wa zamani kwenye nyimbo zao. Kuna shairi lake lingine liitwalo 'Mapenzi Niliyo Nayo', baadhi ya maneno yameandikwa hivi.

"Mchana kutwa nalia, kwa fikirazo benati, Moyo wanichechemea, kwa penzi sili seketi, Mapenzi niliyonayo, kwako hayana kiasi, kwa wingi yamefurika, mapenzi nikupendayo, mwili damu nakauka, haunitulii moyo."

Vipande vya maneno haya, vimewekwa kwenye wimbo wa Super Matimila ya Remmy Ongala, kwenye wimbo wa 'Mariam'.

"Sili nafikiri zaidi kuliko wewe, nakonda kama mnazi kwa mapenzi niliyonayo, moyo wanichechemea, mwili damu nakauka mpenzi ee."

Tukitoka kwa mshairi huyo tunakwenda kwa mshairi na mwandishi maarufu zaidi Afrika Mashariki na Kati, Shaaban Robert. Baadhi ya wanamuziki wamechukua maandishi yake na kuyaweka kwenye nyimbo zao.

Shaaban Dede akiwa na OSS ya Ndekule aliimba wimbo wa 'Nyumba ya Mgumba Haina Matanga'. Maneno mengi ya wimbo ule yametoka kwenye kitabu cha 'Kusadikika' cha Shaaban Robert.

Ni mfalme ambaye alikuwa hana mtoto, ana kila kitu, cheo, pesa, hekima na kila kitu, lakini ugumba umevunja heshima yake. Alikuwa akiwaza na kuwaita waganga wote nchini mwake wamsaidie. Dede naye alichukua baadhi ya maneno na kuyaweka kwenye wimbo wake huo.

"Nimejaliwa elimu iliyonipatia heshima, nina madaraka na uwezo wa kununua chochote duniani, lakini ugumba, umevunja heshima yangu." Ni baadhi ya maneno kwenye wimbo huo, ambayo yamenukuliwa kwenye kitabu hicho.

Juwata Jazz Band wana wimbo uitwao 'Pamela' uliotungwa na Fresh Jumbe. Mtunzi anamwambia mpenzi wake kuwa kadri itakavyokuwa Pamela, wema wake ni wa asili, naye kwa vyovyote atakuwa na la kuiga tu, hivyo hautolingana kamwe. Maneno hayo yanapatikana kwenye kitabu cha 'Adili na Nduguze.'

**Tuma sms 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya siri-12

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AKAZIANGALIA na kuzisoma namba za gari lile kwa kichwa. Akaingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake ya mkononi. Akatafuta picha moja akaiangalia. Ilikuwa ni picha ya gari lile. Na namba zilikuwa ni zile zile. Aliisaka picha nyingine aliyokuwa na wasiwasi nayo. Nayo ilikuwa picha ya gari lile lile. Ni kwa sababu namba zilikuwa ni zile zile. Akatabasamu. Akafungua mlango wa gari yake na kujifanya kama anatafuta kitu ili kusiwe na mtu ambaye atamshuku. Akaufunga na kurejea tena kwenye pub. Akalipita tena gari lile. Akazisoma tena namba, huku kwa uangalifu wa hali ya juu akalipiga picha kwa simu yake ya mkononi.

Picha ya kwanza ilikuwa ni ile aliyoipiga akiwa kwenye geti la nyumba ya marehemu Hafidh Chilambo.

Kulikuwa na magari mawili yaliyokuwa ndani, Toyota Harrier la rangi ya kijivu na nyingine ni Toyota Alphard ya rangi nyeupe. Ya pili ilikuwa ni picha aliyotumiwa na kijana muuza na mkodisha filamu, Nanje.

Siku mbili zilizopita alitumiwa picha ya gari hilo. Eddy alimpa kazi ya kupiga picha gari la mtu ambaye alisimama na Tina siku ambayo alitoka kununua dawa iliyotumika kumuua Chilambo.

Nanje baada ya kusema aliona tukio hilo, akidai Tina alimpa kifuko cha dawa hizo dereva wa gari lililosimama, Eddy alimpa kazi ya kulipiga picha na kumtumia. Kwa bahati nzuri picha zote mbili zilionyesha namba za gari kwa usahihi zaidi. Ndiyo hilo ambalo limepaki nje ya pub ya Fabrice.

"Ina maana mmiliki, au dereva wa gari lile ana uhusiano na familia ya marehemu Chilambo. Na kama Tina alimpa kifuko cha dawa, ina maana binti huyo na jamaa yule aliyeshuka kwenye gari wote wanahusika na tukio hilo. Sasa kwa nini Tina anyongwe peke yake?" Alijiuliza Eddy.

"Hapana, huyu jamaa naye lazima nile naye sahani moja. Na hapa ndipo nitakapopata ukweli wote." Alijiambia.

Ghafla simu yake ikaita. Kwa sababu alikuwa sehemu ambayo alikuwa kikazi, alitaka kuangalia jina la mtu anayepita, badala yake akaiweka mfukoni huku bado ikiwa inalia.

Alichofanya ni kubonyeza kitufe kinachofanya itoe sauti. Badala yake ikawa inatikisika tu bila sauti yoyote. Haraka alitoka eneo hilo na kurejea ndani ya pub hiyo, na moja kwa moja akaelekea msalani, ili kuzuga.




**"Nusu niondoke. Maana nimeingia huku nimeangalia wee, napiga simu haipokelewi, nikasema kanidanganya nini, wewee." Alilalamika Mwahija kwa sauti nyingine kabisa ndogo, ya poa, lakini ya kudeka akiwa kifuani mwa Eddy, ambaye sasa alikuwa na uhakika kuwa aliyekuwa akipiga muda si mrefu uliopita alikuwa yeye.**

Aliporejea na kutaka kwenda sehemu ambayo alikuwa amekaa, kabla hajafika alikutana na mwenyeji wake. Mtu aliyemwita wakutane pale.

"Mwenzangu vipi, nimepiga sana simu haipokelewi. Nimeingia humu nimetafuta wee mpaka watu wananishangaa."

"Na wengine wakakuita uende ukakae walipo." Eddy alidakia.

"Kama ulikuwepo." Alijibu Mwahija huku akiangua kicheko.

"Waambie washindwe na walegee, hukuwaambia kuwa una mtu?"

"Mmhh, wanywaji wanajua hilo, wao wakimuona mwanamke tu, basi macho juu, hawajui kama wa nani, kaitwa na nani, jamani."

"Tena mrembo kama wewe, ndiyo kabisaa"

Wakati wakiongea maneno hayo, Eddy na Mwahija walikuwa katikati ya pub hiyo ya Fabrice. Mwahija alionekana malaika hasa.

Weupe wake, uliokolezwa na taa za rangi mbalimbali, zilizidi kumfanya awe mrembo zaidi. Gauni alilovaa la kisasa, ambalo unaweza kudhani ni mwanamitindo lilimfanya awe anatazamwa na kila anayekutana naye, awe mwanaume au mwanamke.

Macho yake na tabasamu lake, vilizidi kumfanya aonekane wa pekee.

Eddy alimkumbatia, na Mwahija akakubali kukumbatiwa. Hakuna aliyeongea kwa sekunde kadhaa, huku mioyo yao ikiongezeka kasi ya kudunda.

"Samahani mpenzi, nilikuja mapema kidogo, ila nilitoka kwenda kwenye gari yangu, baada ya kukumbuka kuwa sikutia loki milango." Eddy alidanganya.

"Nusu niondoke. Maana nimeingia huku nimeangalia wee, napiga simu haipokelewi, nikasema kanidanganya nini, wewee." Alilalamika Mwahija kwa sauti nyingine kabisa ndogo, ya poa, lakini ya kudeka akiwa kifuani mwa Eddy, ambaye sasa alikuwa na uhakika kuwa aliyekuwa akipiga muda si mrefu uliopita alikuwa yeye.

"Usijali, hebu tutoke hapa, twende kule ambako mimi nilikuwa nimekaa, hapa kila mtu anatuangalia sisi, utafikiri wao hawana wapenzi." Alijibu na yeye kwa sauti ndogo ya kubembeleza, maneno ambayo yalimfanya Mwahija kuangua kicheko kifupi.

Walishikana mikono na kwenda kukaa sehemu ambayo awali Eddy alikaa.

"Karibuni, sijui mlihitaji vinywaji gani?" Walishtuliwa na sauti ya mhudumu wa kike aliyekuwa amesimama mbele.

"Hebu msikilize mgeni wangu hapa." Eddy aliutupa mpira kwa Mwahija.

"Naomba soda, chips na mayai mawili."

"Hallo, kumbe hunywi wewe?"

"Kwani hata soda si nakunywa?"

"Nauliza pombe, hapa ni baa bibie."

"Walaa, sinywi pombe mimi na sijawahi."

"Na wewe kaka mkubwa?"

"Naomba ndizi mbili za kukaangwa na kuku wa kuchoma. Pia maji chupa moja kubwa."

Dakika kumi baadaye vyakula vilikuja na wawili hao wakaanza kuviteketeza matumboni mwao, wakishushia na vinywaji walivyoagiza.

"Mwahija ujue nakupenda sana?"

"Sijui."

"Unajua." Alijibu Eddy na kama kawaida Mwahija huwa anapenda sana kucheka.

"Umejuaje kama najua?"

"Binadamu tuna lugha ya mwili, isingewezekana mimi siku ile nikutoe pale ofisini, tuzurure kwa miguu hadi kwa marehemu Chilambo. Halafu mimi nikuite leo hadi huku, kisa tu nije niongee na wewe tu basi. Kwa hiyo hata mwenyewe moyoni mwako, utajua tu kama nakuhitaji."

"Sawa, ila nyinyi wanaume tabia zetu, naweza kukukubalia hapa, halafu ukishafanikiwa tu, hata simu hopokei tena."

Ilikuwa ni zamu ya Eddy kukauka kwa kucheka, halafu akamjibu "Tatizo Mwahija, kosa la mtu mmoja usitake kuliunganisha kwa mtu mwingine."

"Danny wewe mimi nawajua wanaume tabia zenu." Ndipo Eddy akakumbuka kuwa siku ya kwanza alipofika kwenye duka la dawa la kina Mwahija alijitambulisha kwa jina la Danny.

"Hebu nipe nafasi mimi utaona kitu kingine tofauti."

Mwahija alishusha pumzi kwa nguvu na kutulia tuli. Kwa uzoefu ya Eddy ilimpa picha kuwa tayari ameshamaliza kazi hiyo. Wala hakuwa na haja ya kuumuliza kama amekubali au la.

Kwa muda mrefu hakuwa na mpenzi yeyote. Na hii ilitokana na kukabiliwa na kazi nyingi ambazo zilimfanya kuhamahama huku na huko, kiasi cha kumfanya asitulie na kutafuta mwanamke mmoja akatulia naye.

Hata hivyo, ndani ya nafsi yake, alitokea kumpenda Mwahija siku ya kwanza tu alipomuona. Hakutaka kumpoteza hata chembe, licha ya kwamba alikwenda pale kikazi.

Ni msichana aliyeweza kukidhi vigezo vyote anavyohitaji, ikiwamo moyo wake kusuuzika kila anapomuona.

Siku zote moyo ukipenda, hakuna kiungo chochote cha mwili kinachoweza kuuzuia.

"Tunaenda nyumbani kwangu leo?"

ITAENDELEA JUMAPILI



# IDADI YA WATOTO ANAOTAKA VERA SIDIKA

KUTOKA 254 Kenya, Mrembo na mfanyabiashara Vera Sidika, ameweka wazi idadi ya watoto anaotaka kuwa nao kwenye maisha yake ambao ni watoto watatu au wanne.

Vera Sidika ameshea hilo kwenye Insta Story yake baada ya shabiki kumuuliza amepanga kupata watoto wangapi.

Mrembo huyo pia ameeleza kwamba huenda mwishoni mwa mwaka huu 2022 akaongeza mtoto wa pili.

Vera kwa sasa ana mtoto mmoja wa kike aitwaye Asia Brown aliyempata na mpenzi wake Brown Mauzo.



# WHOZU

## AELEZA UKWELI WA CHANZO CHA KUMFICHA MWANAYE

KWA mara ya kwanza msanii Whozu 'Don Dingoo' amenyoosha maelezo ya chanzo cha kumficha mtoto wake Lola.

Whozu amezaa na mrembo Cappuccino Tunda ambapo kwa muda mrefu wamemficha mtoto wao huyo.

Whozu juzi alishea video clip ya mtoto wake kwenye page ya Instagram kisha kuandika ujumbe ufuatao.

"Lola mrembo wangu baba yako nilikuficha sana nilitaka ukue vizuri ila walimwengu bahati mbaya wamenizidi nguvu, sisi tumeshaamua kumtegemea Mwenyezi Mungu tu".

"Nikwambie tu mwanangu Instagram ni maisha ya teknolojia utasifiwa, utatukanwa, utaambiwa kila kitu, hilo wala lisikuumize kichwa kwanza sio shida zako mwanangu. Mimi baba yako nipo nyuma yako kwa lolote lile".

# Joh Makini alivyomvaa Sallam Sk Twitter, soma hapa

UNAIKUMBUKA Don't Bother ya Joh Makini ft AKA? unaambiwa wimbo huo umezua maneno huko Twitter baada ya Meneja wa Diamond Platnumz Sallam SK kusema ameunganisha ngoma hiyo kufanyika bila malipo yoyote.

Joh Makini aka-comment kwenye post hiyo kwa kusema Sallam aelezee ameiunganisha vipi kwani alipambana sana kukwamisha wimbo huo usifanyike.

"Aelezee aliunganisha vipi yeye sio chanzo cha hiyo collabo, kwa mazingira niliyofanya collabo na AKA nitawashukuru sana Nikki wa Pili na G NakoWarawara lakini waliomleta walikua hawataki itokee".

"Muarabu alipambana sana kukwamisha hii basi tu Mwenyezi Mungu hajawahi kushindwa" ameandika Joh Makini juzi.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTEGA POGBA
MANCHESTER United imempa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28 mkataba ambao utamfanya alipwe mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki ili kusalia katika klabu hiyo. ***(Sun)***

### SAVIC ANUKIA UNITED
MANCHESTER United wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Lazio na Timu ya Taifa ya Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 26. ***(Calciomercato)***

### GAVI NEEMA YAMFIKIA
KLABU ya Liverpool ipo tayari kumpa kiungo wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Gavi mwenye umri wa miaka 17 karibu pauni 80,000 kwa wiki ili kunasa saini yake. ***(El Nacional - via Mail)***

### SANCHEZ ATAKIWA EVERTON
KLABU ya Everton imepewa ofa ya mshambuliaji wa zamani wa Arsenal na Manchester United, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 33, kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Sun)***

### CHRISTENSEN NJIA MOJA
MAZUNGUMZO ya Chelsea ya kurefusha mkataba wa Andreas Christensen (25), yamegonga mwamba kwa mara nyingine, huku Barcelona wakionyesha ishara ya kutaka kumnunua mlinzi huyo wa Denmark mwezi huu wa Januari. Mkataba wa nyota huyo na Chelsea utamalizika majira ya joto. ***(Gianluca Di Marzio)***

### BARBOSA ATAKIWA EPL
KLABU ya West Ham imefanya mazungumzo na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Barbosa mwenye umri wa miaka 25 kutoka Flamengo. ***(Sky Sports)***

### ROMA YAMTAKA NILES
AS Roma imewasilisha dau la kumsajili kiungo wa kati wa England, Ainsley Maitland-Niles mwenye miaka 24 kwa mkopo kutoka Arsenal hadi mwisho wa msimu na chaguo la kumnunua msimu wa joto. ***(Athletic)***


### PATTERSON HUYO EVERTON
MLINZI wa Scotland, Nathan Patterson (20), anajiandaa kufanya vipimo vya matibabu na Everton baada ya Rangers kukubali dau la awali la pauni milioni 12, ambalo huenda likaongezeka hadi kufikia pauni milioni 16 ikijumuishwa na marupurupu mengine. ***(Football Insider)***

### SUAREZ KUMFUATA MESSI
MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 34, anataka kuondoka Atletico Madrid wakati mkataba wake utakapokamilika msimu wa joto kwa matumaini ya kujiunga tena na Lionel Messi katika klabu ya Paris St-Germain. ***(El Nacional)***

### RENATO ATAJWA MILAN
AC Milan wanafanya mazungumzo na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 24 kutoka Lille. (Calciomercato)

### BOTMAN APANDA THAMANI
KLABU ya Newcastle imeongeza dau lao kwa mlinzi wa Lille, Sven Botman mwenye umri wa miaka 21. ***(Newcastle Chronicle)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HATIMA YA RONALDO MIKONONI MWA KOCHA

## Mreno huyo asema anasubiri kufahamu mwalimu gani atapewa mikoba ya...

**MANCHESTER, England**

JOTO linazidi kuongezeka ndani ya klabu ya Manchester United chini ya kocha wa muda, Ralf Rangnick kuhusiana na hatima ya mshambuliaji wa timu hiyo, Cristiano Ronaldo.

Manchester United walimtangaza, Richard Arnold kuwa Ofisa Mtendaji mpya wa klabu hiyo akichukua nafasi ya Ed Woodward ambapo ataripoti katika majukumu yake kuanzia Februari Mosi, mwaka huu.

Kwa mujibu wa ESPN, kikosi cha Mashetani Wekundu hao kimeshagawanyika na wachezaji hawana umoja kama timu, hali hii inatajwa kuwa ni miongoni mwa sababu zinazoifanya timu hiyo kucheza chini ya kiwango licha ya Ole Gunnar Solskjaer kuondolewa.

Wapo wanaoenda mbali zaidi wakidai mbinu anazotumia Rangnick, haziwapendezi wachezaji wa timu hiyo na baadhi yao, hawamwamini kocha huyu na wasaidizi wake.

Ronaldo anatajwa kama miongoni mwa sababu za kikosi hicho kugawanyika na kuendelea kupata matokeo yasiyoridhisha.

Ronaldo atamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu ujao ingawa ripoti zinasema, nyota huyo ataamua hatima yake ndani ya Manchester United baada ya kuona kocha mpya atakayepewa mikoba ya kukiongoza kikosi hicho.

Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno alirejea Machester United akitokea Juventus ya Italia na tangu atue Old Trafford amefunga mabao mbalimbali yaliyoisaidia timu hiyo kupata pointi muhimu msimu huu.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 823

MECHI KALI
LYON
VERSUS
PARIS ST GERMAIN
1 | 3.49
X | 3.92
2 | 1.91

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# SALAH KUCHUANA NA MESSI TUZO ZA FIFA

**NYON, Uswisi**

MOHAMED Salah ameingia kwenye tuzo za Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), na atachuana na mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or, Lionel Messi na mshindi wa Globe Soccer Award, Robert Lewandowski.

Tuzo za FIFA "Best Awards" zinapigwa na mashabiki kwa asalimia 25, asilimia zinazobaki zinapigwa na makocha wa timu za taifa, manahodha na waandishi wa habari za michezo duniani.

Juzi Ijumaa FIFA walitangaza majina ya wachezaji ambao watawania tuzo hizo ambazo zitafanyika Januari 17, mwaka huu.

Salah amekuwa namba tatu kati ya Messi na Lewandowski pia wachezaji wengine waliotajwa ni Erling Haaland, Kylian Mbappe na Jorginho.

Lewandowski ndiye anayeshikilia tuzo hiyo kwa sasa ambapo alichukua mbele ya Cristiano Ronaldo na Messi.

Kwa upande wa wanawake mshambuliaji wa Chelsea, Sam Kerr ameungana na wachezaji wa Barcelona, Alexia Putellas na Jenni Hermoso kuwania tuzo hio.

Putellas ana tuzo ya Ballon d'Or aliyoshinda mwaka jana.

# Coutinho rasmi Aston Villa




**LONDON, England**

KLABU ya Aston Villa imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa Barcelona, Philippe Coutinho, kwa mkataba wa mkopo wa miezi sita mpaka mwisho wa msimu huu.

Aston Villa wamepewa uchaguzi wa kumnunua moja kwa moja baada ya mkopo kukamilika na watalipa asilimia 50 ya mshahara wake pamoja na bonasi kipindi chote cha miezi sita atakachokuwapo Villa Park.

Coutinho alitua jijini Birmingham baada ya saa 48 kukamilisha vipimo vya afya na utaratibu wa vibali vya kufanyia kazi nchini humo.

Coutinho na kocha wa sasa wa Villa, Steven Gerrard walicheza pamoja kwa misimu miwili na nusu wakiwa Liverpool na sababu hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa nyota huyo kujiunga na klabu hiyo.

Philippe alisajiliwa Barcelona mwaka 2018 akitokea Liverpool kwa dau lililoweka rekodi ya klabu hiyo lakini alishindwa kufanya vizuri Camp Nou kutokana na majeraha.

,998,440

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 9/1/22 | 16:30 | Cagliari vs Bologna | 3.15 | 3.30 | 2.27 |
| 2. 9/1/22 | 16:30 | Torino vs Fiorentina | 2.56 | 3.41 | 2.66 |
| 3. 9/1/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Reims | 2.42 | 3.14 | 2.99 |
| 4. 9/1/22 | 17:30 | Hertha BSC vs FC Koln | 2.66 | 3.46 | 2.51 |
| 5. 9/1/22 | 19:05 | Nantes vs Monaco | 3.22 | 3.27 | 2.23 |
| 6. 9/1/22 | 20:15 | Malaga vs Sporting Gijon | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 7. 9/1/22 | 20:30 | Alaves vs Athletic Bilbao | 3.25 | 3.05 | 2.35 |
| 8. 9/1/22 | 20:30 | Roma vs Juventus | 3.07 | 3.31 | 2.31 |
| 9. 9/1/22 | 20:30 | Genoa vs Spezia | 2.28 | 3.29 | 3.14 |
| 10. 9/1/22 | 22:30 | Ponferradina vs Zaragoza | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 11. 9/1/22 | 23:00 | Villarreal vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 9/1/22 | 23:30 | Las Palmas UD vs Almeria | 2.76 | 3.05 | 2.56 |
| 13. 9/1/22 | 23:30 | Belenenses vs FC Arouca | 2.57 | 3.02 | 2.82 |

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 09 /01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3320 | Empoli vs Sassuolo | 2.51 | 3.71 | 2.56 |
| 14:30 | 3773 | Venezia vs AC Milan | 5.59 | 3.99 | 1.59 |
| 15:00 | 3696 | Brest vs Nice | 2.94 | 3.39 | 2.32 |
| 15:30 | 1145 | Luton Town vs Harrogate | 1.38 | 4.64 | 7.31 |
| 16:00 | 1755 | Aris Salonica vs Atromitos | 1.43 | 4.14 | 7.49 |
| 16:00 | 3327 | Goeztepe vs Antalyaspor | 2.12 | 3.40 | 3.25 |
| 16:00 | 3775 | Boluspor vs Balikesirspor | 1.37 | 4.33 | 7.31 |
| 16:00 | 3871 | Kayserispor vs Altay | 2.22 | 3.36 | 3.07 |
| 16:00 | 4444 | Ionikos Nikea FC vs Apollon Smyrnis | 2.00 | 3.16 | 3.85 |
| 16:00 | 4518 | Rayo Vallecano vs Betis | 2.49 | 3.37 | 2.76 |
| 16:30 | 2044 | Cagliari vs Bologna | 2.91 | 3.36 | 2.39 |
| 16:30 | 5549 | Torino vs Fiorentina | 2.61 | 3.41 | 2.61 |
| 17:00 | 1547 | West Ham vs Leeds | 1.85 | 3.55 | 3.94 |
| 17:00 | 2325 | Metz vs Strasbourg | 4.08 | 3.58 | 1.85 |
| 17:00 | 2352 | Charlton vs Norwich City | 3.75 | 3.46 | 1.93 |
| 17:00 | 2769 | Cardiff vs Preston | 2.25 | 3.30 | 3.05 |
| 17:00 | 2819 | Liverpool vs Shrewsbury | 1.22 | 6.37 | 9.95 |
| 17:00 | 3347 | Montpellier vs Troyes | 1.60 | 3.94 | 5.39 |
| 17:00 | 4002 | Wolverhampton vs Sheffield Utd | 1.65 | 3.74 | 4.92 |
| 17:00 | 4585 | Clermont Foot vs Reims | 2.41 | 3.08 | 3.08 |
| 17:00 | 5102 | Stoke City vs Leyton Orient | 1.36 | 4.63 | 8.08 |
| 17:00 | 5180 | Tottenham vs Morecambe | 1.07 | 9.92 | 24.79 |
| 17:30 | 1412 | Hertha BSC vs FC Koln | 2.69 | 3.44 | 2.48 |
| 18:15 | 1289 | Volos vs Panathinaikos | 3.50 | 3.26 | 2.07 |
| 18:15 | 3205 | Sevilla FC vs Getafe | 1.58 | 3.66 | 6.42 |
| 18:30 | 2143 | Portimonense vs Maritimo | 2.20 | 3.15 | 3.30 |
| 18:30 | 4515 | Napoli vs Sampdoria | 1.46 | 4.62 | 6.22 |
| 19:00 | 1125 | Eyupspor vs Genclerbirligi | 1.86 | 3.32 | 3.85 |
| 19:00 | 1241 | Cameroon vs Burkina Faso | 1.62 | 3.57 | 5.75 |
| 19:00 | 5473 | Caykur Rizespor vs Besiktas | 3.06 | 3.40 | 2.20 |
| 19:05 | 3665 | Nantes vs Monaco | 3.23 | 3.28 | 2.22 |
| 19:30 | 1486 | VfL Bochum vs VfL Wolfsburg | 3.33 | 3.48 | 2.10 |
| 20:10 | 5422 | Nottingham vs Arsenal | 5.10 | 3.77 | 1.63 |
| 20:15 | 5716 | Malaga vs Sporting Gijon | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 20:30 | 2111 | AEK Athens vs PAOK | 2.24 | 3.16 | 3.21 |
| 20:30 | 3056 | Genoa vs Spezia | 2.22 | 3.30 | 3.25 |
| 20:30 | 3890 | Osasuna vs Cadiz CF | 1.75 | 3.46 | 5.02 |
| 20:30 | 4198 | Alaves vs Athletic Bilbao | 3.75 | 3.25 | 2.06 |
| 20:30 | 4328 | Olympiakos vs Asteras Tripolis | 1.26 | 5.52 | 9.86 |
| 20:30 | 4742 | Roma vs Juventus | 3.16 | 3.30 | 2.27 |
| 21:00 | 3767 | Benfica vs Pacos Ferreira | 1.18 | 6.53 | 13.85 |
| 21:00 | 4004 | Sporting Braga vs Famalicao | 1.41 | 4.44 | 7.10 |
| 22:00 | 5394 | Ethiopia vs Cape Verde | 4.36 | 3.17 | 1.90 |
| 22:30 | 3913 | Ponferradina vs Zaragoza | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 22:45 | 1751 | Lyon vs Paris St Germain | 3.49 | 3.92 | 1.91 |
| 22:45 | 2536 | Verona vs Salernitana | 1.39 | 4.89 | 7.39 |
| 22:45 | 5566 | Inter vs Lazio | 1.43 | 4.88 | 6.37 |
| 23:00 | 4747 | Villarreal vs Atletico Madrid | 2.75 | 3.20 | 2.60 |
| 23:30 | 3300 | Las Palmas UD vs Almeria | 2.71 | 3.05 | 2.61 |
| 23:30 | 5846 | Belenenses vs FC Arouca | 2.70 | 3.05 | 2.65 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KIPA NAMUNGO AFUNGUKA WATAKAVYOIDHIBITI SIMBA

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

KIPA chaguo la kwanza la Namungo FC, Jonathan Nahimana, amesema kikosi chao hakina hofu ya kukutana na Simba katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi kwa sababu wanaufahamu ubora na udhaifu wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Namungo itakutana na Simba katika mechi ya hatua ya nusu fainali itakayochezwa kesho usiku wakati mapema jioni Azam FC watavaana na mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Yanga.

Nahimana aliliambia gazeti hili wachezaji wote wa Namungo wako tayari kwa mchezo huo na wanaimani watapambana ili kupata ushindi katika mchezo huo na kusonga mbele.

Mrundi huyo alisema malengo yao ni kucheza fainali hali ambayo inawafanya wajipange kwenda kucheza kwa 'jihadi' bila kujali wanakutana na klabu hiyo kongwe.

Alisema hawana ugeni na Simba kwa sababu wamekutana nao mara kwa mara katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na hivyo wanafahamiana vizuri kimbinu na ufundi.

"Kwetu ni vizuri kwa sababu tunakutana na timu ambayo tunajuana, nina imani utakuwa mchezo nzuri na kuvutia kwa sababu kila mmoja anahitaji kupata matokeo mazuri, hatutarudi makosa tuliyofanya kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara na hatuwadharau Simba, ina wachezaji wazuri na wana uwezo wa kutafuta matokeo," alisema Nahimana.

Aliongeza amejiandaa kukutana na ushindani katika mechi hiyo kwa sababu kila timu inahitaji kufikia malengo kwa kutinga fainali na kubeba ubingwa.



Mshambuliaji wa Namungo, Obrey Chirwa (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Azam FC katika mechi ya michuano ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa Alhamisi kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar. Azam ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Hitimana aziwaza pointi sita

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

MIPANGO! Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amesema ameanza mikakati ya kusaka pointi sita kuelekea mechi zake mbili za Ligi Kuu Bara zinazofuata ambazo ni dhidi ya Tanzania Prisons na Mbeya Kwanza.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Hitimana alisema malengo yake makubwa kuhakikisha anapata pointi hizo sita na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi.

Hitimana alisema ataendelea kukiimarisha kikosi hicho na kurejesha makali yake kama ilivyokuwa katika msimu uliopita ingawa anafahamu ligi hiyo ina ushindani na changamoto mbalimbali.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa ukizingatia kila timu imejipanga vizuri na yoyote anayeshinda anapanda nafasi ya juu, tunahitaji kutoka hapa tulipo sasa, inatulazimu kupata pointi muhimu dhidi ya wapinzani wetu," alisema Hitimana.

Alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanaongeza umakini na kuhakikisha wanakuwa watulivu wakati wote wanapofanya mashambulizi.

"Tunapambana kufanyia kazi madhaifu yetu ili kuhakikisha mzunguko unaofuata hatukosei, hatutaki kupoteza pointi katika mechi zetu tukianzia na michezo miwili inayokuja," alisema kocha huyo.

# Michezo

Jumapili Januari 9, 2022

Nipashe



## Hatima ya Ronaldo mikononi mwa kocha

HABARI UK 21



Kiungo wa Simba Queens, Joelle Bukuru (kulia), akipambana kumtoka mchezaji wa Yanga Princess, Janeth Christopher katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Simba Queens ilishinda mabao 4-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Etop safi Msimbazi

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba aliyekuja kwa majaribio, Udoh Etop, ameonekana kukubalika mapema na wadau wa soka wa timu hiyo licha ya kupewa dakika chache kuonyesha uwezo wake.

Etop ambaye alionekana kulimudu vyema eneo la kati, ni mchezaji mwenye nguvu na anayejua kukaa mahali sahihi akiwa na asipokuwa na mpira.

Hata hivyo, hatima ya nyota huyo pamoja na Msudan Sharaf Eldin Shiboub na winga Cheikh Moukoro kutoka Ivory Coast zitajulikana baada ya Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco kuwasilisha ripoti yake kwa mabosi wa klabu hiyo.

Pablo aliliambia gazeti hili anashirikiana na uongozi kuhakikisha wanapata mchezaji mwenye uwezo mkubwa wa kucheza nafasi ya kiungo ili kuongeza nguvu kwenye kikosi cha timu hiyo.

"Kila mchezaji anayekuja viongozi wanakuwa wamenipa taarifa, tutawaangalia na yule ambaye atakuwa na vigezo ninavyovitaka tutamwongeza katika kikosi chetu," alisema Pablo.

Aliongeza bado ni mapema kusema lolote kuhusiana na wachezaji hao waliokuja kwenye majaribio kwa sababu anahitaji muda zaidi kujiridhisha.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try again' alisema watamsajili mchezaji yoyote ambaye kocha atakuwa amevutiwa naye ili kuhakikisha wanaimarisha kikosi chao na kufikia malengo waliyoyaweka.

# SIMBA, YANGA ZILIVYOKAMATWA

### Hata hivyo Bara bado tishio katika michuano ya Mapinduzi ambayo...

**Adam Fungamwango na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea visiwani hapa, juzi zilikutana na wakati mgumu zilipokuwa zinacheza mechi zao za mwisho za hatua ya makundi.

Mapema jioni, Yanga ilikubali kulazimishwa sare ya jioni ya mabao 2-2 dhidi ya vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wakati sare ya bila kufungana ilikuwa ni matokeo yaliyowakutanisha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba dhidi ya Mlandege.

Hata hivyo, Yanga iliyomaliza ikiwa na pointi nne kinara wa Kundi B, pointi sawa na Simba iliyokuwa Kundi A, zilisonga mbele katika michuano hiyo kwa kuzifuata Azam FC na Namungo kutoka Kundi A.

Ratiba ya michuano hiyo inaonyesha mechi ya nusu fainali ya kwanza itakuwa kati ya Azam FC dhidi ya Yanga wakati Namungo itawakaribisha Simba katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya pili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wachezaji wa KMKM wana uzoefu na uwezo mzuri wa kusakata kandanda kama walivyo nyota wa timu yake na kupelekea mchezo wao kuwa na ushindani wakati wote.

Kaze alisema alijua anaenda kukutana na timu nzuri na kubwa kwa upande wa Zanzibar, hivyo aliwaandaa wachezaji wake kuongeza umakini na utulivu kila walipokuwa wanamiliki mpira.

"Tumecheza na timu iliyosheheni wachezaji wenye uzoefu, ni timu kubwa, ndio maana tulikuwa tunacheza kwa tahadhari katika mchezo huo, hatukuwadharau kwa sababu na wao ni wakubwa," alisema Kaze.

Aliongeza kwa upande wa kikosi chake ameweka wazi hawakucheza vizuri katika kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili walibadilika na walifanikiwa kupata magoli.

"Tumecheza vizuri lakini KMKM nao walicheza vizuri, walicheza kwa kujilinda na kushambulia kama ilivyokuwa kwetu sisi, kikubwa tumefanikiwa kuingia nusu fainali, tutaendelea kujipanga ili tutimize malengo yetu," Kaze alisema.

Hata hivyo Mrundi huyo ambaye amerejea Jangwani kwa mara ya pili alilalamika waamuzi waliochezesha mechi yao walishindwa kutafsiri vyema sheria za mchezo huo.

"Ikiwa wanahitaji kuboresha mashindano haya lazima pia waboreshe na waamuzi, walete waamuzi wenye viwango na uzoefu wa mechi kama hizi ambazo ni ngumu," alisema kocha huyo.

Kwa upande wake Kocha Msaidizi wa KMKM, Salum Ali Salum, alisema licha ya kutolewa katika michuano hiyo lakini kikosi chake kimefanya vizuri na wanastahili kupongezwa.

"Tumecheza michuano hii bila kufungwa, tumetolewa kwa tofauti ya goli moja, sasa ni muda wa kujipanga na michezo ya Ligi Kuu Zanzibar, lengo letu lilikuwa ni kuchukua ubingwa, ila haikuwa bahati yetu, hata hivyo wachezaji wangu wanastahili pongezi kwa uhodari waliouonyesha kwenye mashindano haya," alisema Salum.

Naye Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, alisema mchezo wao dhidi ya Mlandege ulikuwa mgumu lakini umewasaidia kuendelea kujiimarisha kuelekea michezo ya Ligi Kuu Bara na hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Pablo alisema wapinzani wao walicheza mfumo wa kukaba zaidi na 'kufunga njia' zote na kuufanya mchezo kuwa mgumu zaidi.

Mhispania huyo alisema wapinzani wao walicheza kwa vurugu na rafu za mara kwa mara dhidi ya wachezaji wake, hadi muda mwingine kufanya vitendo ambavyo havikuwa vya kimpira.

Kocha wa Mlandege, Abdulaziz Bakechi, alisema timu yake ilicheza kwa kujituma ili ipate nafasi ya kusonga mbele katika michuano hiyo lakini bahati haikuwa upande wao.

"Tulihitaji alama tatu ili tusonge mbele, tulicheza na timu kubwa, ingawa tulicheza kwa bidii kubwa kwa ajili ya kusonga mbele, mipango yetu haikufanikiwa, tunarudi kujipanga na mechi za ligi, naamini wachezaji wangu wameimarika na watarejea na elimu fulani," Bakechi alisema.

Fainali ya mashindano hayo yaliyoshirikisha timu 10 kutoka Bara na Visiwani na yanayofanyika kila mwaka itachezwa ifikapo Januari 13, mwaka huu.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, SL P 9